
SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Aliyekutwa** amelala juu ya mti Masasi arudishwa Mbeya
UKURASA 3



**Hatimaye Dembele kubakia Barcelona**
UKURASA 21


# Nipashe

Jumamosi Desemba 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580805
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Hatimaye Sirro akunjua makucha

• **Atoa** maagizo tisa kwa polisi, yamo ya rushwa, matumizi ya nguvu, ubambikaji kesi... *Endelea ukurasa 2*

Uongozi na wafanyakazi wa The Guardian Limited wanawatakia wasomaji na wadau wetu heri ya KRISMASI na Mwaka Mpya



Anna Msumba akipamba kibanda cha mfano wa mahali alipozaliwa Yesu Kristo katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Albano, Dar es Salaam jana kwa maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Msako nyumba kwa nyumba aliyetupa kichanga

UKURASA 3




## Chanjo ya corona makanisani Krismasi

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAIBADILISHIA GIA BIASHARA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Hatimaye IGP akunjua makucha

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Siro, ametaja mambo tisa ya kufanya ili kuongeza kasi ya utendaji katika jeshi hilo, ikiwamo kutumia lugha za staha kwa wateja wa ndani na nje ya jamii ya jeshi hilo.

Akizungumza jana wakati wa kufunga mafunzo ya kozi ya uongozi katika kambi ya Kamba Pori wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, IGP Sirro alisema lugha zisizo na staha zinaweza kusababisha migogoro na kukosekana kwa haki.

IGP Sirro alisema kuwa pamoja na kuacha lugha hizo, pia ni lazima kuacha kula rushwa na kupoteza haki kwa wahusika kwa kuwa itajenga chuki kwa jeshi hilo na kukosekana kwa maadili kwa mujibu wa sheria.

"Toeni elimu kwa wananchi juu ya madhara ya uhalifu, wapo wengine wanafanya makosa kwa sababu ya kukosa elimu, hivyo tujitahidi kutoa elimu ya mara kwa mara itakayosaidia wananchi kuchukia uhalifu," aliagiza.

Alisema wananchi wanapaswa kusikilizwa na kupata haki zao zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa nchi huku akiwataka askari wa jeshi hilo kuacha matumizi ya nguvu kupitiliza.

"Hakuna haja ya kutumia nguvu za ziada kama hakuna uhitaji. Kwa trafiki (Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani) hata kama mtu anakosa barabarani, mpe onyo na si kutumia lugha chafu pamoja na kupokea rushwa, hili linalichafua Jeshi la Polisi, pia muwe kimbilio la jamii katika kuwasikiliza na kutatua matatizo yao.

"Kuna ugonjwa mwingine umezuka wa wapelelezi kuwabambikizia kesi wananchi kutokana na kupokea kitu kidogo (rushwa). Hii inasababisha walio na hatia kuachiwa huru, hali ambayo inachangia visasi, chuki na hata kusababisha mauaji kwa mwenye haki," alionya.

Vilevile, alitoa rai kwa viongozi wa shule hiyo kuendelea kuweka utaratibu mzuri wa kutoa mafunzo kwa askari walioko kazini, lengo likiwa la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mkuu wa Shule ya Polisi Moshi, Ramadhan Mungi, alisema walipokea wanafunzi 1,712 na waliohitimu ni 1,697 huku 15 wakiachishwa masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utovu wa nidhamu na maradhi.

"Kwa mwaka 2021, tumetoa mafunzo kwa awamu tatu kwa ngazi ya ukoplo na kwa na jumla ya koplo 8,171, ambao watakwenda kuongeza nguvu katika vituo vyote vya polisi na utendaji utaongezeka," alibainisha.

Baadhi ya viongozi wa dini waliokuwapo katika sherehe hizo, akiwamo Daniel Amani, Msimamizi wa Kanisa Katoliki lililoko ndani ya shule hiyo, aliwataka kuwa na nidhamu, kuongeza maadili na kusimamia misingi ya sheria bila kumsahau Mungu.

"Nidhamu katika majukumu yenu itasaidia utendaji kazi wenu kuwa na ufanisi mkubwa, ichukieni rushwa, acheni kutumia nguvu za ziada sehemu ambayo hazihitajiki, tendeni haki, mtafika mbali zaidi," alisema.



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia) akisisitiza jambo wakati alipokuwa akizungumza na Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM Komodoo Azana Hassan Msingiri (katikati) mara baada ya kumjulia hali Mzee Hassan Omar Mzee aliyelazwa katika Kituo cha Afya Kibweni wilaya ya Magharibi"A" Mkoa wa Mjini Magharibi (kushoto) ni Kamanda Mwashamba Mbarouk Salum. PICHA: IKULU

## Chanjo UVIKO-19 yafikishwa sokoni

**Na Mary Geofrey,** IKUNGI

WATAALAMU wa Afya, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wametembea Soko la Ikungi mkoani Singida kwa lengo la kuhamasisha na kutoa chanjo ya UVIKO-19.

Wataalamu hao walitoa huduma hiyo jana ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya 'Kuhamasisha na Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19 katika Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili' unaoendelea kutekelezwa nchi nzima na Wizara ya Afya kupitia kitengo cha Elimu kwa Umma.

Mtaalamu wa Ufuatilia na Udhibiti wa Magonjwa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, akizungumza na wafanyabiashara katika soko hilo, alisema lengo la serikali ni kuwakinga Watanzania dhidi ya madhara yatokanayo na virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19.

Aliwataka wananchi hao kutumia fursa hiyo kuuliza maswali na kupatiwa majibu yaliyo sahihi yatakayowapa nafasi ya kufanya uamuzi sahihi wa kujikinga wao na familia zao dhidi ya UVIKO-19.

Alisema kampeni hiyo inalenga kuwafikia watu 3,000 wa mkoa wa Singida, hivyo ni wajibu wa wananchi kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kwa kupata chanjo.

"Wananchi hawana shida, wanahitaji elimu, waliopata elimu wanachanja. Changamoto ipo kwa watoa huduma hawaendi kuwafuata wananchi kwenye maeneo wanamoishi au wanakofanyia shughuli zao," alisema Dk. Nzobo.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Dk. Gatete Mahava, alisema wilaya yake imepangiwa kuchanja wananchi 600 kulingana na idadi ya wananchi wake.

Alisema wameweka malengo mbalimbali ya kuwafikia wananchi, kutumia wataalamu wa afya ambao watafika katika maeneo ya watu na kuwapa huduma hiyo.

Mtoa huduma za afya wilaya ya Ikungi, Agnes John, alisema amefika katika soko hilo kwa ajili ya kutoa huduma ya chanjo na alifanikiwa kuchanja wananchi wengi kwa wakati mmoja tofauti na alivyokuwa akiwasubiri kituoni.

"Nimegundua wananchi wanataka kufuatwa katika maeneo yao. Tumekuja hapa tumewaeleza faida za chanjo na kuondoa dhana mbaya walizonazo vichwani na wakakubali kuchanja kwa hiari," alisema Agnes.

Mfanyabiashara katika soko hilo, Sebastian Mathias, aliwashukuru wataalamu wa afya kwa elimu waliyotoa na kushawishika kupata chanjo hiyo.

# Chanjo corona kutolewa makanisani Krismasi

**Na Mary Geofrey,** SINGIDA

MGANGA Mkuu wa Manispaa ya Singida mkoani Singida, Dk. Anuary Milulu, amesema watatumia siku ya Sikukuu ya Krismasi kutembelea nyumba za ibada, masoko, magulio na nyumba kwa nyumba kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kupewa chanjo ya UVIKO-19.

Dk. Milulu aliyaeleza hayo kupitia mkutano wake na wataalamu wa afya katika wilaya hiyo jana muda mfupi kabla ya kuanza kutembea mtaani kuwafuata wananchi ili kuwapatia chanjo ya UVIKO-19 katika kampeni inayoendelea.

Alisema kuwa malengo ya Manispaa hiyo ni kuchanja watu 360 kwa siku katika kutimiza lengo la serikali la kuchanja watu 80,000 hadi 100,000 kwa siku.

Malengo hayo yanatekelezwa kupitia kampeni ya 'Kuhamasisha Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19 katika Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili' unaoendelea kutekelezwa nchini nzima.

Dk. Milulu alisema kupitia mkesha wa Sikukuu ya Krismasi watahakikisha wanawafuata waumini kwenye nyumba za ibada kwa lengo la kufikia watu 3,000 kwa mkoa wa Singida.

"Tumekutana na wataalamu hapa kupeana mbinu za kwenda kutoa chanjo kwa wananchi ili kufikia lengo la serikali. Njia mojawapo ni kutumia magari ya matangazo, hivyo wakati huu wataongeza idadi ya magari ili kuwafikia watu mbalimbali.

Alisema wamejipanga kuchanja watu 360 na awali walikuwa wakichanja watu 100 na mkakati walioweka utawezesha kufikia watu wengi zaidi.

"Hii ni mbinu tu ya kuwafikia hawa watu, tunaamini tukienda na kuwafikia watu tutachanja wengi zaidi," alisema Dk. Milulu.

Mtaalamu wa Ufuatilia na Udhibiti wa Magonjwa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, aliwataka maofisa hao kuwafuata wananchi nyumbani, shambani, ibadani na maeneo mengine ambako wanapatikana.

Alisema lengo ni kufikia malengo ya serikali kwa kuwafuata watu mahali walipo ili wapate chanjo ya UVIKO-19.

Alisema vikwazo vingi vinaweza kutatulika kwa kushirikiana kwa pamoja katika kuendesha kampeni hiyo.

HABARI KITAIFA

# Msako nyumba kwa nyumba aliyetupa kichanga

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WANANCHI wa kijiji cha Chikukwe, Masasi mkoani Mtwara wameanza msako wa nyumba kwa nyumba ili kubaini wanawake wajawazito kwa lengo la kumsaka mwanamke aliyejifungua mtoto na kumtupa jalalani kisha kutoweka kusikojulikana.

Msako huo wa kumsaka mwanamke huyo ambaye bado hajajulikana, ulianza rasmi juzi kijijini hapo na unashirikisha wenyeviti wote wa vitongoji.

Akizungumza jana kuhusu msako huo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Chikukwe, Victoria Msala, alisema baada ya tukio hilo wananchi wamesikitishwa na kitendo hicho cha kikatili.

Alisema kutokana na jambo hilo, uongozi wa kijiji kwa kushirikiana na wananchi, umefanya kikao cha pamoja na kukubaliana kufanya msako kijijini hapo nyumba kwa nyumba kumsaka aliyefanya kitendo hicho.

Msala alisema hatua hiyo itasaidia kubaini nani alikuwa mjamzito na amejifunguaje, hivyo kama yuko mwanamke ambaye amefanya jambo hilo, atabainika na kukamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. "Msako huu tunafanya kupitia kwa wenyeviti wa vitongoji wote kwa kuandikisha watu wao na wanawake wajawazito na tunafanya hivi nyumba kwa nyumba ili kumsaka aliyefanya unyama huu," alisema Msala.

Naye Victor Masaiko ambaye ni Mwenyekiti wa kitongoji cha Mwambao, sehemu ambayo kichanga hicho kiliokotwa, alisema watafanya msako huo usiku na mchana na watashirikiana na wenyeviti wa vitongoji wa vijiji vya jirani pia.

Zawadi Mohamedi, mkazi wa kijiji cha Chikukwe, alisema anaunga mkono msako huo ili kumtafuta mwanamke huyo na iwapo atakamatwa, sheria ichukue mkondo wake.

Stela Kuonewa, Mtendaji wa Kata ya Chikukwe, alisema uongozi wa kata utashirikiana bega kwa bega na wananchi katika msako huo huku akisisitiza kuwa jamii inapaswa kukemea kwa nguvu zote vitendo vya kikatili kwa watoto.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Dk. Festo Dugange, akipanda mti katika shule ya sekondari Ukenyenge wilayani Kishapu, alipowasili kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Aliyekutwa amelala kwenye mti arejeshwa kwao Mbeya

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SAILI Juma (27) mkazi wa Mbeya ambaye mapema wiki hii alilala kitandani nyumbani kwao Mbeya na ghafla akaamkia juu ya mti Masasi mkoani Mtwara akiwa amelala fofo, amesafirishwa kurejea Mbeya.

Juma amerejea nyumbani kwao baada ya kuchangiwa nauli na wananchi wa Mbeya waishio Masasi.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi hao walisema wameamua kumsafirisha baada ya kuguswa na aina ya tukio lililomtokea.

Kesi Mwandisile, mwenyeji wa Mbeya anayeishi mjini hapa, alisema juzi walipata taarifa hizo kwa mtu mmoja mwenyeji wa mkoani kwao kuwa amekutwa amelala juu ya mti akitokea huko bila kujitambua.

Alisema tayari wameshamsafirisha kijana huyo baada ya kupata fedha ambazo wamechangishana ili kumwezesha kurejea Mbeya kwa ndugu zake. Licha ya kuchangishana fedha za kumsafirisha, pia alisema alipewa huduma mbalimbali zikiwamo malazi na chakula.

Mwananchi mwingine wa Mbeya, Faustine Mwakipesile, anayeishi wilayani Masasi, alisema kijana huyo amesafiri na basi la kampuni ya Sajda linalofanya safari kutoka Masasi kwenda Mbeya. Alisema wamestaajabishwa na tukio hilo na kwamba si la kawaida kwa kuwa limevuta hisia kubwa kwa jamii na kuacha maswali mengi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mji Masasi, Leila Kasunguru, alisema ofisi yake imekuwa pamoja na kijana kwa siku mbili huku akipatiwa huduma za msingi kikiwamo chakula.

Alisema ofisi hiyo ilipokea michango iliyofikia Sh. 70,000 kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo wa Mbeya wanaoishi Masasi.

Kasunguru alisema katika fedha hizo, Sh 40, 000 amelipiwa nauli kutoka Masasi hadi Mbeya na Sh.30,000 amekabidhiwa ili kumsaidia akiwa safarini.

Akizungumza na gazeti hili, Juma alisema baada ya kupata fahamu anaendelea vizuri na hakuna kinachomsumbua na kwamba anawashukuru wote waliomsaidia.

"Nawashukuru wote walionisaidia kunishusha juu ya mti na kunipeleka hospitalini na wale walionichangia fedha zinazonifanya leo (jana) nianze safari ya kurudi nyumbani Mbeya," alisema Juma.

Alisema bado hajapata ufahamu hadi sasa nini kilitokea na amewezaje kutoka Mbeya hadi kufika Masasi na kueleza kuwa yote atakwenda kuyajua atakapofika Mbeya.

# Usalama wa magari wahimizwa kuepusha ajali za barabarani

**Na Maulid Mmbaga**

KAMANDA wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, amewataka wamiliki wa mabasi ya abiria kuhakikisha yanakuwa salama kabla ya kuanza safari ili kuepusha ajali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mutafungwa alisema katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, kuna ongezeko kubwa la abiria sambamba na mabasi, hivyo kusisitiza kuwa magari yote yanayotoa huduma hiyo yanapaswa kufuata taratibu zote za usafirishaji.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutafungwa, katika kipindi hiki wanapita katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kukagua mabasi hayo pamoja na kusisitiza uzingatiaji wa sheria za barabarani ili kuhakikisha usalama wa abiria. "Ni kazi yetu ya msingi kupita katika barabara zote kubwa hapa nchini kuona wenzetu maofisa wa ukaguzi na usalama barabarani na askari wengine wanavyotekeleza majukumu yao kusimamia hasa sheria za usalama barabarani," alisema Mutafungwa.

Aliongeza kuwa magari yote yanayoongezeka katika kipindi hiki, wamiliki wahakikishe yamekaguliwa na kuthibitika kuwa yanaweza kufanya safari kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kwa kuwa hawataki kuona ajali zikitokea barabarani.

"Hatutaki kuona gari bovu linatembea barabarani. Tunajua kipindi hiki kila mtu anafikiria kupata fedha hasa wafanyabiashara wa magari ya usafirishaji kupitia wingi wa abiria. Lakini tunahitaji kama ni msafirishajia apate fedha kupitia utaratibu ambao ni mzuri si kwa gharama ya maisha ya watu," alisisitiza.

Pia alibainisha kuwa katika ukaguzi unaoendelea magari tisa yamebainika hayana ubora wa kusafirisha abiria licha ya kwamba yalikuwa yanataka kusafirisha watu, hivyo yalizuiwa hadi yatakapofanyiwa matengenezo.

Aliwataka wamaliki, madereva na mawakala wa mabasi hayo kukutana na kuangalia namna ya kusafirisha abiria ambao walishawachukulia fedha zao kwa kuwapatia usafiri mwingine ambao ni salama.

HABARI KITAIFA

# Babu jela maisha kwa kunajisi mjukuu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu mkazi wa kijiji cha Ruo, Halmashauri ya Mtama, Selemani Matola (53), kutumikia kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumnajisi mjukuu wake mwenye umri wa miaka minane.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mwagala Muyonga, baada ya mshtakiwa kukutwa na hatia kwa kosa lililokuwa linamkabili pamoja na kukiri mbele ya mahakama bila kulazimishwa.

Kabla Hakimu Muyonga kutoa hukumu, alimpa nafasi ya kujitetea na kuiomba mahakama imwonee huruma kwa kutompa adhabu kali kwa madai ni mkosaji kwa mara ya kwanza na kwamba anayo familia inayomtegemea akiwamo mke, watoto watatu na wazazi wawili ambao ni wazee.

Pia mshitakiwa alidai iwapo atapewa adhabu kali, familia itakosa huduma yake ya matunzo, huku akidai ibilisi wa mapenzi alimshawishi kufanya kitendo hicho.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya aina hiyo kwa kuwa kitendo alichofanyiwa mtoto huyo licha ya kwamba kimemuumiza kimwili pia kimemwathiri kisaikolojia.

Mramba pia aliiomba mahakama kuangalia uwezekano wa kumlipa mwathirika wa kitendo hicho kifuta machozi kutokana na maumivu aliyoyapata kutoka kwa mshtakiwa ambaye ni babu yake.

Hakimu Muyonga, akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 72/2021, alianza kwa kukataa utetezi uliotolewa na mshitakiwa kwa kueleza kitendo alichokifanya mshtakiwa si cha kiungwana.

Kwa mantiki hiyo, alisema anamhukumu kwa mujibu wa vifungu vya sheria namba 130 (1) 2 (e) na 131 (1) vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 rejeo 2019 kutumikia kifungo cha maisha gerezani.

Licha ya kutumikia kifungo hicho, pia mahakama ilimtaka mshtakiwa kumlipa mlalamikaji kifuta machozi cha Sh. milioni tatu.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na Mramba kuwa mshtakiwa alifanya unyama huo Desemba 17, mwaka huu usiku wakati mkewe, Somoe Yusufu, alipokweenda kwenye sherehe za ngoma za jadi za watoto wa kaka yake na aliporejea alishangaa kukuta watoto wao wamelala chumbani kwao bila ya baba yao.

Mramba alidai mke alipofuatilia chumba kinachotumika kulala watoto, alimkuta mume wake akiwa amelala huko usingizi mzito na mjukuu wao wakiwa uchi wa mnyama na alipowafanyia ukaguzi, akabaini mbegu za kiume zikiweka michirizi kwenye mapaja ya mjukuu wao, hali iliyomfanya kuwaita majirani na kutoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya kijiji hatimaye polisi.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima (katikati) akikagua nyumba walizokuwa wanaishi watumishi Kiwanda cha Chai cha Mponde (Mponde Tea Estate) kilichopo Bumbuli, wilayani Lushoto, kiwanda hicho kinatarajia kurejesha uzalishaji baada ya kusimamishwa mwaka 2013, kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Kalisti Lazaro na kulia kwake ni msimamizi mkuu wa kiwanda hicho Mhandisi Msemo Temba. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Waziri atoa siku 45 visima vikabidhiwe

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ameupa siku 45 uongozi wa Wilaya ya Mpwapwa kukamilisha usimikaji wa mabomba na matanki ya kuhifadhi maji safi na salama kwenye vijiji vya Mbugani, Ngh'ambi na Kiegea katika wilaya ya Mpwapwa.

Alitoa agizo hilo juzi alipozuru kikazi na kukagua utekelezaji wa mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya ikolojia vijijini ulio chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na unaotekelezwa katika wilaya tano nchini ambazo ni Mpwapwa, Mvomero, Kishapu, Simanjiro na Kaskazini A.

Akiwa wilayani Mpwapwa katika kijiji cha Nghambi, Dk. Jafo alikasirishwa na kitendo cha mkandarasi wa kampuni ya Make Engineering kutoka Dar es Salaam kutokamilisha kwa wakati mradi wa uchimbaji wa visima vyenye urefu wa mita 150 na kumwagiza mkandarasi huyo kukamilisha kazi mapema iwezekanavyo. Waziri huyo alisema azma ya serikali ni kuhakikisha huduma zinasogezwa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

"Natoa siku 45 tu maji yaanze kutoka hapa, mradi huu ukamilike. Wananchi hawa wanataka maji mapema, hakuna kwenda sikukuu na watumishi acheni kukaa ofisini, simamieni hili kikamilifu," aliagiza.

Alitoa rai kwa wakazi wa Mbugani, Ngh'ambi na Kiegea kutumia vizuri mvua inayonyesha kwa kupanda miti kwa wingi ili kulinda mazingira na kusisitiza kuwa agenda ya mazingira ndiyo kipaumbele cha serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Mkuu wa wilaya ya Mpwapwa, Josephat Maganga, alisema atahakikisha ndani ya siku hizo 45 kazi zote zinakamilika na huduma ya maji inatolewa kwa wananchi.

Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini unafadhiliwa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Nchi Maskini kupitia Mfuko wa Dunia wa Mazingira ambapo kuna shughuli za uchimbaji wa visima, ujenzi wa majosho, uchimbaji wa malambo na utengenezaji wa majiko banifu. Jumla ya Sh. 2,257,042,400 (Bil. 2.257) zimeidhinishwa kutumika kugharamia miradi hiyo katika wilaya ya Mpwapwa.

# Agizo zito waliovamia karantini

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wananchi wakiwamo wafugaji waliovamia eneo la kuhifadhia na kuiangalia kwa muda mifugo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi kuondoka mara moja.

Ndaki amewataka wavamizi hao kuondoka eneo hilo kwa hiari huku akionya kuwa atakayekaidi serikali itatumia nguvu kumwondoa.

Waziri Ndaki alitoa agizo hilo juzi alipotembelea eneo la karantini ya Kwala iliyoko katika Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani.

Alisema eneo hilo lina maslahi mapana kitaifa na hivyo wananchi kuvamia na kufanya shughuli zao katika eneo hilo linafanya karantini hiyo kupoteza sifa ya kibiashara kimataifa.

"Hili eneo lina maslahi ya kitaifa, hivyo wananchi walioingia na kukaa huku bila utaratibu wowote tuwaambie waondoke kwa hiyari. Wale tutakaowakuta wakati tutakapoanza kazi ya ujenzi wa karantini ya kisasa basi tutatumia nguvu kuwaondoa", alisema.

Pia alisema mwaka wa fedha ujao watatenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga karantini hiyo ili iwe ya kisasa itakayokidhi matakwa ya biashara ya kimataifa ya kusafirisha wanyama hai kwenda nje ya nchi.

"Hatuwezi kwenda kimataifa bila ya kuwa na kituo hiki, wenzetu wakija hapa ghafla na hali hii watatuambia msiuze ng'ombe wala nyama zenu kwa sababu hakuna mahali watakuwa wamehakikishiwa kuwa wako salama ", alifafanua

Awali, Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Othman Makusa, alimweleza Waziri Ndaki kuwa kituo hicho kina miundombinu duni na kimevamiwa na wananchi kutoka vijiji vya jirani na wanafanya shughuli mbalimbali zikiwamo kilimo, makazi na ufugaji jambo ambalo linasababisha kituo hicho kupoteza sifa za kimataifa za kuwa karantini.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndaki alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, itakwenda kuliainisha eneo hilo vizuri.

Alisema katika kufanya hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi wataambiwa wahame na maeneo mengine yatabakishwa kwa wananchi ili waendelee na shughuli zao.

HABARI KITAIFA

# Dozi 376,000 chanjo ya corona zapokewa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imepokea dozi 376,320 za chanjo aina ya Moderna kupitia mpango wa COVAX zitakazotumika kuchanja wananchi 188,160.

Baada ya kupokea chanjo hizo kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alishukuru mpango wa COVAX ambao umewezesha awamu ya kwanza kwa aina hiyo ya chanjo kuingia nchini.

Alibainisha kuwa mapokezi ya chanjo hizo za jana yanafanya jumla ya chanjo zilizopokewa nchini tangu kuanza kutoa chanjo dhidi ya UVIKO-19 hadi sasa kuwa dozi 6,408,950, zikijumuisha Sinopharm, Janssen na Pfizer, ambazo zinatosha kuchanja jumla ya Watanzania 3,204,475.

"Shukrani za kipekee ziwaendee wadau wetu wa maendeleo hususani katika kujali afya za Watanzania kwa kuendelea kutupatia chanjo ambazo zitatusaidia kuwakinga wananchi dhidi ya Ugonjwa wa Virusi vya Corona (UVIKO-19)," alisema.

Waziri huyo aliwasilisha shukrani zake hizo kwa mpango wa COVAX ukiongozwa na mashirika ya GAVI, WHO na UNICEF kwa kuanzisha mpango huo hususani kwa kuwezesha kupatikana kwa chanjo dhidi ya UVIKO-19.

Alisema serikali itaendelea kutoa chanjo dhidi ya UVIKO-19 katika vituo mbalimbali vya afya nchini kwa mujibu wa miongozo iliyopo, hivyo akawaomba wanaohusika kuwajibika kwa kasi kubwa ili kuwawezesha Watanzania wengi kupata chanjo mapema iwezekanavyo.

Dk. Dorothy alikumbusha kuwa wizara ilishatoa mwongozo wa chanjo unaofafanua vyema taratibu za utoaji wa chanjo hizo wenye lengo la kufikia uchanjaji wa asilimia 60 ya Watanzania.

"Chanjo hizi zipo kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma kuanzia zahanati hadi hospitalini. Ninapenda kusisitiza wale ambao bado hawajapata chanjo, wafanye haraka kupata huduma hii kwa kuwa ugonjwa wa UVIKO-19 upo.

"Ninachukua fursa hii kuwaagiza viongozi na watendaji wa ngazi zote kutoa ushirikiano wa hali ya juu ili kuhakikisha kuwa wananchi wanahimizwa kwenda kwenye vituo vya huduma za afya ili wakapate elimu kuhusu umuhimu wa chanjo na kisha kuchanja.

"Ninawahimiza wananchi kuchukua hatua mbalimbali za kujikinga dhidi ya UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na uvaaji wa barakoa, kunawa mikono kwa maji na sabuni, kutumia vitakasa mikono (sanitizer) na nyinginezo ambazo wataalamu wa afya wamekuwa wakiendelea kuzisisitiza," aliagiza.

Waziri huyo pia aliwaomba wadau wengine wenye nia ya kusaidia eneo hilo kwa namna moja au nyingine, kujitokeza na kufuata utaratibu wa mwongozo wa serikali kuhusu suala la kuwezesha msaada huo.



Waziri wa Madini Dk, Doto Biteko akipokea maelezo ya namna ya ufungaji wa maduara ya uchimbaji wa madani kwa Meneja wa Mgodi wa Ntambalale namba tano Jackson Mahona, wakati alipofanya ziara katika mgodi huo kukagua usalama wa mashimo ya uchimbaji wa madini jana. **PICHA: SHABAN NJIA.**

# 'Mafuriko' abiria yatikisa Moshi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ABIRIA wamefurika kwenye Stendi Kuu ya Mabasi ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wakihangaika kupata magari ya kuwapeleka katika viunga vya mkoa huo baada ya kuwasili kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Nipashe ilishuhudia jana msongamano mkubwa wa watu kwenye stendi hiyo, baadhi ya wazazi na walezi wakiwa na watoto, huku vijana wanaojua kutumia fursa, wakisaidia kubeba mizigo kwa malipo ya kati ya Sh. 500 na 2,000 kwa mizigo midogo na Sh. 4,000 hadi 15,000 kwa mizigo mikubwa.

"Abiria ni wengi, wanatoka mikoani na wengine wapo na watoto na mizigo, hivyo tumelazimika kupandisha bei ili nasi tuweze kujiongezea kipato.

"Tulikuwa tunabeba mzigo kutoa eneo ambalo magari makubwa yanaposhushia hadi kwenye magari ya kwenda Kibosho, Marangu, Himo, Rombo na Mwika kwa Sh. 500 hadi 1,000, pia Sh. 1,500 hadi 2,000, inategemea na ukubwa wa mzigo," alisema Daud Mroso, mbeba mzigo katika stendi hiyo.

Dereva wa Taksi, Simon Patrick, alisema licha ya hali ya maisha kuwa ngumu, kwa wiki hii wameanza kuona fedha.

"Abiria ni wengi, wanapokosa usafiri wa umma hulazimika kukodisha usafiri binafsi hasa wale wanaokuwa na mizigo na watoto, hii kwetu ni neema kwa kweli," alisema.

Baadhi ya abiria, akiwamo Florence Mlay, walisema magari yapo lakini nauli zimepanda, hasa nyakati za jioni huku akiziomba mamlaka husika kufuatilia na kuchukua hatua stahiki dhidi ya kadhia hiyo.

"Mpaka sasa tatizo kubwa linalotukabili kama abiria ni baadhi ya magari kupandisha nauli kimya kimya. Hawatoi risiti.

"Eneo la kwenda kwa Sh. 500 kwa sasa ni Sh. 1,000 na magari mengine yakiwamo ya Rombo, Sanya Juu hayakubali kupakia watu wa njiani na wakikuta kwenye gari hutaka bei ya mwisho wa gari.

"Pia wanahitaji watoto walipiwe au kukuacha stendi kutokana na kuwa na watoto au mizigo mingi," Florence alilalamika.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Kilimanjaro, Paul Nyello, alisema kwa sasa wanaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha hakuna gari lolote litakalopandisha bei na abiria wote wanapata haki zao kwa mujibu wa sheria.

"Tunaomba kunapotokea tatizo lolote la ukiukwaji wa sheria, abiria toeni taarifa na hatua stahiki zitachukuliwa.

"Tumejipanga kukabiliana na matatizo yote hasa msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka," alisema Nyello.

Katika Mji wa Moshi Nipashe ilishuhudia jana kukiwa na foleni ya magari tofauti na ilivyokuwa kabla ya kipindi hiki cha mwishoni mwa mwaka, jambo ambalo limekuwa likishuhudiwa karibu kila mwaka kinapowadia kipindi hiki.

# Chumvi yenye utata yatua kwa mkemia

**Na Thobias Mwanakatwe,** NGORONGORO

SAMPULI ya chumvi ya kulishia mifugo inayodaiwa kuwa feki ambayo inagawiwa bure kwa wafugaji na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), iliyolalamikiwa kwamba inaathiri mifugo, imepelekwa katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Dar es Salaam kwa ajili uchunguzi zaidi.

Sampuli hiyo ilifikishwa jana katika ofisi hizo zilizoko Temeke na nyingine itapelekwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Morogoro kwa ajili ya Morogoro kufanyiwa utafiti.

Maofisa watatu kutoka NCAA akiwamo Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Ngorongoro, Dk Chobi Chubwa, na Diwani wa Ngorongoro, Simon Saitoti, waliungana katika jopo hilo kupeleka sampuli hiyo Dar es Salaam.

Kabla ya kuanza safari, jopo la maofisa hao lilifanya mahojiano na mmiliki wa kampuni ya Panga Building Materials and Company Limited, Mark Panga, ambaye kampuni yake ilipewa zabuni ya kununua chumvi na NCAA. Katika mahojiano hayo, Panga aliwathibitisha maofisa hao kuwa alifuata taratibu zote katika kupata zabuni na kununua chumvi hiyo aliyoinunua Nakuru, Kenya na kabla ya kwenda kununua, aliwashirikisha maofisa wa NCAA ambao walimwonyesha aina ya chumvi inayotakiwa.

Juzi, zaidi ya wafugaji 8,000 wa kata za Ngorongoro na Nainokanoka, Ngorongoro mkoani Arusha, walieleza wasiwasi wao juu ya uwezekano wa ng'ombe wao kupoteza maisha baada ya kupewa chumvi iliyochanganywa na mawe na rangi na mifugo hiyo kila inapoitumia inaharisha.

Chumvi hiyo ambayo imezua utata, inadaiwa imesambazwa kwa wafugaji hao na NCAA ikiwa ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mwaka 2016. Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo kwa NCAA iwe inawapa wafugaji chumvi ya kulisha mifugo pamoja na maji ili wafugaji waache kupeleka mifugo yao ndani ya Bonde la Ngorongoro ambako walikuwa wakifuata chumvi ya asili na maji katika bonde hilo ambayo inasaidia sana kwa afya za mifugo.

Wafugaji wamelalamika kuwa chumvi waliyopewa wiki mbili zilizopita haina viwango ambapo imechanganywa na mawe na rangi na mifugo yao inapotumia inaharisha hali ambayo inahatarisha afya za ng'ombe hao.

Diwani Saitoti, awali akizungumza na gazeti hili, alisema hali siyo nzuri kwa mifugo ya wafugaji wa kata hiyo kwani baada ya kuitumia chumvi hiyo ambayo inadaiwa kununuliwa na NCAA kutoka nchi jirani.

Saitoti alisema katika kata yake ililetwa mifuko 900 ambapo ilikuwa imeshasambazwa kwa zaidi ya wafugaji 5,000 na kubakia sita tu kupitia kwa wenyeviti wa vijiji na kwamba baada ya ng'ombe kuanza kuitumia wakaanza kuona dalili tofauti.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, alisema Jumatatu alifika eneo la tukio katika kata ya Ngorongoro na kuzungumza na wafugaji na kwamba ametoa agizo chumvi hiyo isiendelee kutolewa kwa wafugaji tena na wale ambao wamekwishapewa wasiipe mifugo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi, wachezaji tumieni vyema dirisha dogo la usajili

**WAKATI** mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ukiwa unaendelea, tayari Shirikisho la Soka Nchini (TFF), limeshafungua dirisha dogo la usajili kwa klabu zinazotaka kuimarisha vikosi vyake.

Dirisha hilo lilifunguliwa tangu Desemba 15, mwaka huu na linatarajiwa kufungwa ifikapo Januari 15, mwakani.

Usajili huo wa dirisha dogo unahusisha pia na timu za Ligi ya Championship, First League pamoja na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, lakini tu kwa timu ambazo zilikuwa hazijatimiza idadi ya wachezaji wanaotakiwa kwa mujibu wa kanuni.

Lengo la usajili huo si kutoa nafasi ya kuimarisha vikosi vya timu hizo zinazoshiriki ligi mbalimbali za hapa nchini, ni kutaka kufikia malengo ya msimu husika kwa mwelekeo wa wanaowania ubingwa kuanza kuonekana au kwa wale wanaotakiwa kuanza kupambana kujiondoa mkiani. Kila timu inatakiwa isajili wachezaji kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi ambalo lenyewe ndio linafahamu vyema mapungufu yaliyoko kwenye kikosi husika na si kiongozi wa klabu, mwanachama au shabiki. Mchakato huu unahitaji kufanyiwa kazi kiweledi kwa sababu matokeo yake huonekana hadharani na majibu hupatikana mwishoni mwa msimu, klabu itakayokosea katika zoezi hili, ni wazi itajiweka kwenye wakati mgumu wa kufanya vyema.

Tunatarajia kuona klabu, wachezaji na makocha wanalitendea haki dirisha hili la usajili kwa kila mmoja kufanya majukumu yanayomhusu ili malengo yanayokusudiwa yafikiwe ipasavyo. Kuingilia majukumu ya mwingine, ni moja ya sababu ambayo inaweza kuizamisha timu.

Huku kukiwa na udhamini mnono wa Azam Media ambao umetangaza kutoa zawadi ya fedha mpaka kwa timu itakayonusurika na janga la kushuka daraja, tunatarajia kuona ushindani unaongezeka katika michezo inayoendelea na hatimaye timu itakayostahili kupata ubingwa ipate. Mbali na klabu, wachezaji wanatakiwa kufanya maamuzi sahihi ya kujiunga na timu ambazo zitawapa nafasi ya kuendeleza vipaji vyao na kuacha kuangalia upande mmoja tu wa maslahi.

Hii imewatokea wachezaji wengi wanaokubali kutoka timu A na kujiunga na timu B bila kuangalia hatima yake ya baadaye. Viongozi wa klabu ni kama wazazi, ni vyema mkawa makini katika kusajili wachezaji ambao watatumika na si kuchukua wachezaji ambao uhakika wa kupata namba ni mdogo. Mbaya zaidi usajili huu unawagusa zaidi wachezaji chipukizi wa Kitanzania ambao taifa linawategemea kupeperusha bendera ya nchi katika mashindano mbalimbali yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Nipashe tunazikumbusha klabu zinazowasajili nyota chipukizi, lakini wanakosa namba kwenye timu hizo, kuwatoa kwa mkopo kwa klabu nyingine ili kuendeleza vipaji vyao badala ya kuwaacha wakikaa benchi kwa muda mrefu au kuacha kuwasajili kwa 'mihemko'.

Tunaamini soka la sasa ni la ushindani, na ili mchezaji aonyeshe kiwango bora au akabiliane na ushindani kutoka kwa timu pinzani ni lazima apate nafasi ya kucheza mara kwa mara, kumsajili mchezaji bila ya kumhakikishia nafasi ya kucheza ni kutomtendea haki maana kipaji chake kitakuwa kimejiweka njia panda. Si lazima kila mchezaji asajiliwe timu kubwa au kongwe, mchezaji anayejituma anaweza kuonekana na mawakala na makocha wa nje ya nchi endapo atapata nafasi ya kucheza kwa sababu michezo yote ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara inaonekana kwenye televisheni.

Mchezaji kama Ditram Nchimbi akiwa Polisi Tanzania alikuwa ni tegemeo, lakini aliposajiliwa Yanga, kwake nafasi ya kucheza ilikuwa adimu na hivyo kupoteza namba hadi kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), lakini baada ya 'kuzinduka' na kukubali kuondoka klabuni hapo kupitia dirisha dogo la usajili lililofunguliwa, amekuwa ni mchezaji muhimu ndani ya kikosi cha Geita Gold FC ambacho kilikuwa na hali mbaya kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara. Huu ni wakati wa kila mmoja kutafakari kabla ya kukubali kusaini mkataba wa kujiunga na timu yoyote katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wanaosajiliwa Simba SC, Yanga wajiandae kisaikolojia

**HIKI** ni kipindi cha usajili wa dirisha dogo, klabu mbalimbali zinasaka wachezaji ambao wataongeza makali kwenye timu zao. Tumeona baadhi ya wachezaji wakitoka klabu hii kwenda nyingine. Katika kipindi hiki mpaka sasa Geita Gold imeonekana haitaki mzaha, kwani imeonekana kulitumia vizuri dirisha hili kwa kuwanasa William Lucian 'Gallas', Juma Nyosso, Ditram Nchimbi kutoka Yanga, na hadi jana ilikuwa kwenye hatua ya mwisho kukamilisha usajili wa Kelvin Yondani kutoka Polisi Tanzania.

Sijaona pilikapilika sana kwenye klabu ya Simba kutaka kusajili wachezaji wa Kitanzania. Inawezekana ina mpango huo, lakini inafanya kwa siri. Watani zao wa jadi, Yanga ipo kwenye hatua za mwisho kuwatangaza wachezaji Salum Aboubakar 'Sure' Boy' kutoka Azam na Dennis Nkane wa Biashara United.

Inavyoonekana ni suala la muda tu, kwani tayari meneja wa 'Sure Boy', Heri Mzozo, amethibitisha mchezaji huyo 'ameshaanguka' mkataba wa miaka miwili kwa Wanajangwani hao, huku Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso akikiri walikuwa katika mazungumzo na Yanga kwa ajili ya kukamilisha 'dili' la Nkane, mmoja wa wachezaji chipukizi na machachari.

Wote hao ni wachezaji wazuri, lakini linapokuja suala la kwenda Simba au Yanga kinakuwa ni kitu kingine kabisa.

Hapa simsemi Nkane na Sure Boy, peke yao, hata wachezaji wengine wa Kitanzania watakaosajiliwa na Yanga, na wale ambao tunawasikia wakisajiliwa Simba, wakae wakijua kwenda kwenye timu hizo si sawa na kujiunga na Mtibwa Sugar, Polisi Tanzania, Geita Gold, Kagera Sugar, Prisons au timu nyingine.

Nikiandika hivi kuna ushahidi mwingi uliowahi kutokea nyuma na sasa, jinsi wachezaji waliovuma kwenye klabu mbalimbali, lakini wakaenda kukwama kwenye klabu hizo kubwa. Hapo ndipo utawakumbuka kina Hussein Javu, Said Bahanuzi, Paul Nonga, Waziri Junior na wengine wengi ambao walifanya vyema sana kwenye klabu zao walizotoka, lakini walipofika Yanga walishindwa kuonyesha kiwango hata kile kile tu.

Kwa upande wa Simba, walisajiliwa wachezaji kama, Issa Rashid 'Baba Ubaya', Novatus Lufunga, Juma Luizio, Charles Ilamfya na wengine ambao hawakufurukuta kama ilivyokuwa walikotoka.

Siyo wachezaji wote wanaosajiliwa na timu hizo huwa hawafanyi vyema, la hasha, ila kumekuwa na wimbi la baadhi ya wachezaji kushindwa kabisa kuonyesha viwango vyao wakiwa kwenye timu kubwa, hasa za Simba na Yanga.

Hapo ndipo zinaanza kuja zile dhana za imani za kishirikina kwa wachezaji wenyewe na baadhi ya mashabiki. Ukiangalia kwa undani utakuta hakuna 'misumari', ila kuna vitu ambavyo wachezaji hao wanakutana navyo. Na hata kina Nkane watakutana navyo, hivyo wajiandae tu kisaikolojia. Kujiweka vizuri kisaikolojia ndiko kutakakowafanya wawe kwenye viwango vyao, ili baadaye wasije tena kutolewa kwa mkopo.

Kwanza wajue wanakwenda kucheza kwenye timu zenye mashabiki wengi ambao hawana simile. Wanachotaka wao ni ushindi na mchezaji awe kwenye kiwango kile kile mara nyingi zaidi kuliko kuwa chini ya kiwango.

Wanachotakiwa kukifanya ni kufanya mazoezi mara mbili zaidi kuliko timu walizotoka, kwani sasa watakuwa wanakamiwa zaidi na timu watakazocheza nazo. Ni tofauti na walipokuwa wanacheza huko walikotoka, waliweza kuonyesha uwezo kwa sababu walichukuliwa poa na wachezaji wa timu pinzani, lakini sasa wapo Simba au Yanga ni mwendo wa kukamiwa mwanzo hadi mwisho, hivyo kama mchezaji hana pumzi, stamina na mazoezi ya kutosha, hawezi kupambana.

Mchezaji akiwa Simba au Yanga, hata kama uwezo wake ni kawaida, kutokana na maneno na kusifiwa na mashabiki anaweza kujiona uwezo wake ni mkubwa mno na kuanza kuvimba kichwa, kumbe kiuhalisia sivyo hivyo, badala yake uwezo unapungua siku hadi siku.

Hata Sure Boy, akae akijua pamoja na kwamba Azam ni timu kubwa, lakini anatakiwa kubadilika, Yanga haiwezi kuwa sawa na Azam kwa mashabiki.

Mara nyingi mchezaji akiwa Azam au timu nyingine anaweza kukosea mara nyingi, kukosa mabao mara nyingi, lakini kwa sababu haangaliwi inaonekana kawaida, lakini aina hiyo hiyo akiyakosa akiwa Simba au Yanga mjadala unaanza. Hivyo ndivyo maisha yalivyo kwenye klabu hizi kubwa ambazo wachezaji wanaosajiliwa watakwenda kukutana nayo, kwa hiyo wajiandae kisaikolojia, kukabiliana na kelele za kushangiliwa na kuzomewa na mashabiki, kuhimili presha hizo, kufanya mazoezi mara nyingi zaidi kuliko yale ya timu walizotoka kwa sababu watakamiwa sana, lakini pia wasitarajie kuingia tu watapata namba kirahisi, badala yake watatakiwa kutokwa machozi, jasho na damu ili kupata muda wa angalau kwanza kuingia kipindi cha pili, kabla ya kupata namba ya kudumu baadaye.

# Wachimbaji wamlilia waziri ujenzi wa choo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo katika mgodi wa Ntambalale ulioko kijiji cha Wisolele, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameangua kilio mbele ya Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, kuomba awasaidie kupata huduma ya vyoo kwa kuwa wamekuwa wakijisaidia vichakani.

Kilio hicho walikitoa jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika mgodi wa Ntambalale namba mbili muda mfupi baada ya Waziri huyo kufanya ziara ya kukagua usalama na hali ya uchimbaji mgodini hapo huku akiambatana na Kamishna wa Tume ya Madini, Janeth Reuben.

Mmoja wa wachimbaji hao, Nestory Masale, alisema mgodi huo hauna huduma ya vyoo kwa ajili ya wachimbaji na wageni wanaowatembelea na badala yake wanajisaidia vichakani. Alisema hali hiyo inatishia kuwapo magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.

Naye Stephen Kasiga alisema uchimbaji wa madini unatakiwa kwenda sambamba na afya njema kwa wachimbaji na kama huduma ya choo inakosekana, kunaweza kutokea magonjwa ya mlipuko kwa wachimbaji, hivyo kushindwa kufanya uzalishaji na serikali ikakosa mapato.

Baada ya kusikiliza jambo hilo, Waziri Biteko alisema hawezi kuzungumzia suala hilo kwa sababu linaweza kutatuliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Charles Fussi, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga.

Pia alisema sehemu ya migodi midogo ambayo halmashauri inachukua mapato kwa mujibu wa sheria ndogo walizojiwekea, mkurugenzi anatakiwa kutatua changamoto zinazopatikana maeneo hayo ikiwamo ujenzi wa barabara ili aendelee kukusanya kodi bila malalamiko ya wachimbaji.

Dk. Biteko aliwapongeza viongozi wa mgodi huo kwa kujenga zahanati ya kijiji ambayo inatumika kuwahudumia wachimbaji wanaopata matatizo wakiwa kazini pamoja na wananchi wanaozunguka mgodi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Kiswaga, alitoa muda wa siku 14 wenyeviti wa wachimbaji wadogo na wamiliki wa leseni kuhakikisha wanajenga vyoo haraka na baada ya muda huo ataanza kukagua mgodi mmoja baada ya mwingine kuangalia kama huduma hiyo ipo.

# Walengwa TASAF walalamikia kukosa dawa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WALENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini kwa awamu ya tatu unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mkoani Shinyanga, ambao wana Bima za Afya za CHF iliyoboreshwa, wamedai kunyimwa huduma za afya.

Imedaiwa kuwa wanapokwenda kupatiwa matibabu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, hunyimwa dawa, hivyo kwenda kununua kwenye maduka ya watu binafsi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, alibainisha hayo jana wakati akifungua kikao cha kujadili mafanikio na changamoto za utekelezaji wa mpango huo mkoani Shinyanga, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi 2020.

Alisema moja ya kero kubwa ambazo zimekuwa zikiwakabili walengwa wa mpango huo ni kunyimwa dawa katika vituo vya afya wale wenye kadi za CHF iliyoboreshwa.

"Kumekuwa na malalamiko kwa walengwa wa TASAF wenye kadi za CHF kuwa wanapokwenda kwenye zahanati na vituo vya afya, hawapati huduma wanayotarajia na wamekuwa wakinyimwa dawa na kulazimika kwenda kununua kwenye maduka ya watu binafsi," alisema Omary.

"Lakini akija mgonjwa mwenye fedha taslimu, anapewa dawa. Kitendo hiki kinakwamisha sana juhudi za serikali kuhamasisha wananchi wote wakate bima hii ya CHF iliyoboreshwa sababu ya huduma mbovu, hivyo waratibu wa CHF tatueni changamoto hii," aliongeza.

Kuhusu mafanikio ambayo yamefikiwa na mpango huo, alisema kaya 24,600 zimejiunga kwenye CHF iliyoboreshwa na kaya 22,411 zimeanzisha miradi ya kujikwamua kiuchumi huku zingine 4,119 zikiimarisha makazi yao na zingine kupata milo mitatu kwa siku.

Pia alisema kwa walengwa wa TASAF ambao vidole vyao havitambuliwi na mashine za kielektroniki kwa ajili ya malipo na wasio na vitambulisho ya taifa, waendelee kulipwa kwa njia ya kawaida wakati taratibu za kutatua kero hiyo zikiendelea ili wapate fedha zao na kuondokana na umaskini.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Shinyanga, Dotto Maligisa, alisema katika utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini wa TASAF III awamu ya pili, kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2023), kaya 14,785 zimekidhi vigezo na kuingizwa kwenye mpango na kaya 7,155 zilikosa sifa na kuondolewa.

Baadhi ya waratibu wa TASAF ngazi ya halmashauri, walitaja baadhi ya changamoto ambazo zinawakabili kwenye utekelezaji wa mpango huo kuwa ni baadhi ya walengwa kutokutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa, hivyo kuendelea kukabiliwa na umaskini.



Mbunge wa jimbo la Morogoro mjini, Abdulaziz Abood (katikati) pamoja na Diwani wa kata ya Mbuyuni, Samwel Msuya (kulia) wakifurahia hatua ya ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa nane ya shule mpya ya sekondari Magadu/Buyuni, iliyopo Manispaa ya Morogoro kupitia fedha za mradi wa Covid -19 zilizotolewa na Serikali Kuu alipofanya ziara jana ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa ujenzi huo. **PICHA NA ASHTON BALAIGWA.**

# Mbunge amshukuru Rais ujenzi madarasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na mkakati wa kuboresha sekta za jamii ikiwamo ya elimu kwa kuipatia Manispaa ya Morogoro Sh. bilioni 1.3 kupitia fedha za mradi wa COVID-19 kwa ajili ya kujenga shule mpya sita za sekondari na vyumba vya madarasa katika shule 20 za sekondari .

Abood alitoa shukrani hizo baada ya ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na majengo ya shule mpya za sekondari zilizoko Manispaa ya Morogoro.

Kujengwa kwa vyumba hivyo na shule, alisema kutapunguza kero kwa wanafunzi hasa wa kidato cha kwanza ambao wanatarajia kuanza masomo Januari, mwakani.

"Nikiwa Mbunge wa Morogoro Mjini, nachukua nafasi hii kumshukuru Rais kwa kufanya jambo kubwa sana ambalo kwa mimi nikiwa mbunge kwa awamu hii ya tatu, sijawahi kuona jambo kama hili likifanyika. Tunaendelea kumwombea afya njema ili afanye mengine zaidi," alisema.

Mbunge huyo aliwataka walimu, kamati za usimamizi wa miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na watendaji wa mitaa na kata, kuwa makini na matumizi ya fedha hizo.

" Nitoe rai kwa wote wanaosimamia miradi hii kuwa makini na matumizi ya fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa haya. Mzione za moto kwani ufuatiliaji wake ni mkubwa, alisema Abood.

Pia aliwataka wakuu wa shule na kamati za ujenzi kuhakikisha wanawasimamia makandarasi waliopewa kazi ili ujenzi wake uwe umekamilika kabla ya kumalizika kwa mwezi huu na kukabidhi majengo hayo kwa ajili ya kutumiwa.

Ofisa Elimu Taaluma Sekondari Manispaa ya Morogoro, Jaribu Malambughi, alisema Manispaa hiyo ilipokea Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 86 vya madarasa na kabla ya kujengwa kwa vyumba hivyo, kulikuwa na upungufu mkubwa .

Malambughi alisema mwaka ujao wanatarajia kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 8,292 ambao wanahitaji vyumba vya madarasa 163 na kabla ya kujengwa, madarasa mapya, yaliyokuwepo yalikuwa 124 .

"Ujenzi huu wa vyumba vya madarasa 86 kwa maana hiyo sasa upungufu wa vyumba katika shule za sekondari ndani ya Manispaa ya Morogoro umeisha," alisema Malambughi.

Malambughi alisema majina ya wanafunzi wa kidato cha kwanza yameshatangazwa na hivyo kuwataka wazazi kuwaandaa watoto kuingia madarasani Januari 2022 na hakuna mchango wowote.

# Ulinzi mkali Krismasi, Mwaka Mpya

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la polisi Mkoani Mwanza limesema limeimarisha ulinzi katika nyumba za ibada na kumbi za starehe na maeneo mengine,ili kukabiliana na uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alisema kuanzia jana askari walianza kunzunguka na mbwa, pikipiki, magari na kutembea kwa miguu ili kuimarisha doria kukabiliana na magenge ya kihalifu yaliyojipanga kutekeleza njama zao ovu.

'Wazazi wahakikishe wanakuwa makini na watoto wao katika kusherehekea sikukuu, hususani barabarani, sehemu za michezo, beach, mialoni, kwenye bembea na wanapokwenda kwenye mkesha, wasiache nyumba zao bila uangalizi," alisema Ng'anzi.

Ng'anzi pia aliwataka madereva wa vyombo vya moto, kuendesha kwa umakini na kuhakikisha hawajalewa au mwendo kasi, wakibainika hatua za kisheria zitachukuliwa na wale walio na tabia ya kuchoma matairi barabarani watashughulikiwa.

Alisema wageni wanaotembea mkoani hapa, wananchi wasiwe na hofu kwa kuwa polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wameimarisha vyema ulinzi kwa raia na mali zao.

"Wananchi amani inalindwa kwa kushirikiana, hivyo toeni taarifa kwa askari wetu endapo mtaona viashiria vya uvunjifu wa amani na uhalifu vinapo jitokeza ili vidhibitiwe mapema," alisema Ng'anzi.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia) akikagua eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya kujenga Karantini mpya ya Kwala alipotembelea eneo hilo lililopo katika wilaya ya Chalinze, mkoani Pwani Desemba 23, 2021. Akiwa katika eneo hilo alisema kuwa wananchi wote waliovamia eneo hilo waondoke kwa hiyari vinginevyo shughuli za ujenzi zitakapoanza wataondolewa kwa nguvu. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Waziri ataka teknolojia kisasa utafiti maji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewagiza wataalamu wa maji nchini kutumia teknolojia ya kisasa katika kufanya utafiti ili kupata maji ya uhakika hasa maeneo yenye kero ya huduma hiyo.

Aweso alitoa agizo hilo jana mkoani hapa alipokuwa akifungua Jukwaa la Pili la Wadau wa Sekta Mtambuka wa Bonde la Wami Ruvu.

Waziri alitolea mfano wa baadhi ya wilaya ambazo zimekuwa na kero ya muda mrefu ya maji na wananchi kulalamika zikiwamo Buhigwe mkoani Kigoma na Gairo, Morogoro.

Alisema kutokana na kuwapo kwa kero ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwenye maeneo mengi nchini, serikali imetenga Sh. bilioni 17 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa na ujenzi wa miundombinu ya maji ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama.

"Kwa sasa tunataka mageuzi ya haraka fedha hizi nyingi zilizotolewa lazima zionyeshe mapinduzi katika sekta ya maji. Tunataka wananchi wanufaike na rasilimali maji," alisema.

Pia alisema Tanzania haina umaskini katika suala la maji kutokana na kuwapo kwa vyanzo vingi ambavyo vikisimamiwa ipasavyo, vitawezesha upatikanaji wa maji kuwa wa uhakika zaidi.

Aliwataka wataalamu hao hasa, katika bonde la Wami Ruvu, kutumia taaluma zao katika kutatua kero ya ukosefu wa maji badala ya kubaki ofisini kuchezea kompyuta.

Pia aliwataka kuhakikisha wanawashirikisha wananchi kwenye kulinda na kutunza vyanzo vya maji kwa kuwapa elimu kwamba wanajamii kama hawatashirikishwa kazi zao zitakwama.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau, Julius Mtui, alisema bado kumekuwepo na tatizo la upatikanaji wa takwimu za maji chini ya ardhi kutokana na ushirikiano hafifu baina ya watafiti na taasisi zinazoshughulikia rasilimali maji.

Alishauri kuelekeza nguvu kwenye uchimbaji visima, ujenzi wa mabwawa ya utunzaji wa maji katika kukabiliana na ukosefu au upungufu wa maji kama ilivyotokea hivi karibuni.

Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mariam Mtunguja, alisema kuna haja ya kuunganisha nguvu ya pamoja kwa kuwashirikisha wananchi katika utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kupanda mazao yanayoendana na utunzaji mazingira huku wakifuata sheria.

## Waonywa matumizi mabaya ya mtandao

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WANAVYUO nchini wametakiwa kutumia kwa usahihi mitandao ya kijamii na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha ukatili.

Wito huo ulitolewa jana mjini hapa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jinsia, kutoka Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Mwajuma Magwiza, wakati akizungumza na wanavyuo mbalimbali mkoani hapa kuhusu mwongozo wa uanzishwaji wa madawati ya jinsia vyuoni.

Alisema wanafunzi wengi wanaingia kwenye matatizo ya kudhalilishwa kutokana na kutumia vibaya mitandao ya kijamii, hivyo kusababisha wengi wao kupata matatizo ya kisaikolojia na hata wengine kukatisha uhai wao.

"Wizara tumeona tuje na mifumo mbalimbali ikiwamo kuanzisha madawati haya na tunaendelea kuweka mifumo hii maeneo mengi ikiwamo vituo vya mabasi, sokoni na maeneo yote ya wazi ili kupambana na vitendo vya ukatili," alisema.

Magwiza alisema jukumu la kulinda watoto, kujilinda na kuhakikisha amani ya nchi ni jukumu la kila Mtanzania na sababu za ukatili zilizoainishwa zinaweza kusimamiwa, hivyo kuzuia madhara ikiwamo mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Awali, akiwasilisha mwongozo wa kuanzisha na kuendesha dawati la jinsia katika vyuo vya elimu ya juu na ya kati kwa wanafunzi hao, Ofisa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Alex Shayo, alisema lengo ni kutekeleza kwa pamoja jitihada za kuondokana na vitendo vya ukatili vyuoni.

Shayo alisema mwongozo huo utawezesha wahusika kutoa taarifa katika dawati ili hatua zichukuliwe dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo.

Baadhi ya wanachuo walisema mwongozo huo utawasaidia kujua namna ya kupata na kutoa taarifa za ukatili, hivyo kutoa suluhisho la ukatili vyuoni kwa kuwa awali wanafunzi wengi walikuwa wanakosa sehemu sahihi ya kutoa taarifa kuhusu vitendo hivyo.



## HABARI DODOMA

## Ujenzi wa barabara sasa kufungua fursa

**Na Paul Mabeja,** IRAMBA

SERIKALI kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imetenga Sh. bilioni 7.3 kwa ajili ya kufungua barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Iramba mkoani Singida ikiwa ni utekelezaji wa kaulimbiu yake ijulikanayo kama 'Tunakufungulia Barabara Kufika Kusikofikika'.

Akiwa katika ziara ya kikazi wilayani humo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Raia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alisema azma ya serikali ni kufungua barabara za vijijini ili wananchi wafanye kazi zao bila kikwazo cha usafiri.

Akikagua barabara ya Shelui - Tintigulu yenye urefu wa kilomita saba, Waziri alielekeza barabara hiyo ijengwe kwa ubora unaotakiwa ili idumu na kuwasaidia wananchi katika shughuli zao za kila siku.

"Lengo la serikali ni kuwafungulia wananchi wa vijijini barabara ili isiwe kikwazo tena katika shughuli zao na hapa nimeona baada ya barabara hii kukamilika inakwenda kufungua na kurahisisha mawasiliano ya kata tatu na vijiji sita," alisema

Pia Waziri Ummy alimwelekeza Meneja wa TARURA Wilaya ya Iramba, Mhandisi Evance Kibona, kuhakikisha wanafanya usanifu wa Daraja la Nshoka linalounganisha kata za Shelui - Tintigulu ili barabara hiyo inayojengwa iweze kuleta manufaa kwa wananchi wa maeneo hayo.

"Nimekagua ujenzi wa barabara,umeanza lakini nimeona kuna mto Nshoka ambao unatakiwa kujengewa daraja ili barabara hii inayojengwa iweze kuleta manufaa, vinginevyo bado watakuwa wanapata usumbufu wakati wa mvua nataka tumalize kabisa changamoto hii.

"Mto huu ni mkubwa na hakuna daraja sasa wakati wa mvua wananchi hawawezi kupita hapa, hivyo ni vyema hapa pakajengwa daraja ili barabara hii iwe na tija stahiki, hivyo wahandisi anzeni kufanya usanifu na muingize kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 tuweke ujenzi wa daraja hili kwenye bajeti yetu," alisema

Awali Mhandisi Kibona alisema ujenzi wa barabara hiyo ulianza Desemba 11 na utakamilika Juni, 2022.

Pia alisema barabara hiyo itakayokuwa na urefu wa kilomita saba itagharimu Sh. milioni 524 na inajengwa kwa kiwango cha lami.

# CCM yaonya wanaopanga safu za uongozi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewaonya makada wake ambao wameanza kujipangia safu ya viongozi kabla ya muda wa uchaguzi wa ndani ya chama na jumuiya zake unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali Mstaafu Ngemela Lubinga, alitoa onyo hilo juzi jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha Baraza Kuu la Jumuiya ya Wazazi ya chama hicho.

"Mwaka 2022 ni mwaka wa uchaguzi wa ndani ya chama na jumuiya zake. uchaguzi maana yake ni mfumo wa jamii ya kistaarabu kupata uongozi, kuendesha jumuiya na kwa lugha ya kisiasa ni sehemu ya demokrasia," alisema.

Kanali Lubinga alisema chama kina imani uchaguzi huo utaendeshwa kwa ustaarabu na kanuni za chama na jumuiya lakini kampeni zake bado muda na wakati ukifika watu watataarifiwa na wote ni lazima wazifuate.

"Iko minong'ono miongoni mwenu mmeanza kupiga kampeni hii ni kinyume cha maadili ya chama chetu na jumuiya. Kibaya zaidi tunasikia watu wanabeba viongozi na wengine wameishaanza kutoa rushwa na kupokea ni vema ukaacha wala usithubutu hakuna kisichofahamika.

"Simu yangu inazo WhatsApp zenye ushahidi na Katibu Mkuu wetu wa CCM anafahamu yote. Chama kimelazimika kufanya mabadiliko ya viongozi kutokana na mwenendo usioridhisha na hakitasita kuchukua hatua," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Dk. Edmund Mndolwa, alisema jumuiya imejipanga kulipa madeni mbalimbali ambayo imekuwa nayo pamoja na kushughulikia migogoro ya mipaka ya shule zake.

"Kutoka sasa kila fedha tutakazopata tutatoa asilimia na kuweka fungu la kulipa madeni. Haiwezekani tunasemwa huko nje hatulipi madeni, tuna wastaafu wetu tuna wajane tuna mazungumzo na serikali hili lifanyike," alisema.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Gilbert Kalima, alisema wataendelea kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha makusudio yanayohitajika ndani ya jumuiya yanafikiwa.

Katibu wa NEC Organaizesheni, ambaye ni mlezi wa jumuiya hiyo, Moudline Castico, aliwashukuru viongozi mbalimbali wa jumuiya hiyo kwa kusimamia mambo ikiwamo katika uchaguzi wa ubunge na udiwani.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ummy Mwalimu akiwa na baadhi ya viongozi wa wilaya ya Iramba mkoani Singida akikagua ujenzi wa barabara ya Shelui - Tintigulu yenye urefu wa kilomita saba inayojengwa kwa kiwango cha lami na wakala wa barabara mijini na vijijini TARURA. **PICHA PAUL MABEJA**

# Bil. 12/- zatolewa mikopo makundi maalum

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHILINGI 11,920,750,969 zimetolewa kwa ajili ya kuyawezesha kiuchumi makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika halmashauri saba za mkoa wa Dodoma.

Hayo yalibainishwa juzi jijini hapa na Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alipokuwa akizungumza katika kikao cha Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi cha kutathimini utekelezaji wa sera ya uwekezaji wananchi kiuchumi.

Kikao hicho pia kiliwashirikisha wanawake wajasiriamali, wenye ulemavu na wadau mbalimbali wa masuala ya maendeleo.

Alisema fedha hizo zilizotolewa kwenye makundi hayo katika Halmashauri za Bahi, Chamwinio, Chemba, Dodoma Jiji, Kondoa, Kondoa mji, Kongwa na Mpwampwa.

Alisema Sh. 7,004,724,612 zilielekezwa kwa vikundi vya wanawake, Sh 4,264,231,059 kwa vikundi vya vijana na Sh. 652,795,298 kwa vikundi vya watu wenye ulemavu.

" Kutokana na fedha hizo, jumla ya wanawake 12,427 wamenufaika huku wanaume wakiwa ni 2,249."alisema

Akizungumzia urejeshaji wa mikopo, Dk. Mganga alisema wanawake wameonyesha kuwa na ufanisi mkubwa katika kurejesha mikopo ambapo ni asilimia 43, wakifuatiwa na watu wenye ulemavu kwa asilimia 35 na vijana kwa asilimia 28.

Dk. Mganga alisema tathimini inaonesha kuwa fedha zilizotolewa kwenye makundi hayo zimeelekezwa kwenye miradi mbalimbali ikiwamo ya viwanda vidogo vya machinjio ya kuku, kukamua Mafuta ya alizeti,mkusaga unga wa sembe, kutengeneza majiko banifu na mama lishe.

"Fedha hizi zilizotolewa kwa vikundi vya wanawake, walemavu na vijana zimesaidia upatikanaji wa mikopo kwa makundi ambayo hayawezi kukopesheka kupitia taasisi za fedha.

"Pia mikopo hii imeleta mafanikio makubwa katika uchumi wa wanawake kwa wanawake wengi kujiajiri, kuboresha maisha yako binafsi wa kuwa wanapata fedha za ziada kupitia biashara zao na kuongeza idadi ya wanawake wanaojiunga na bima ya afya,"alisema.

Katibu tawala Msaidizi anayeshughulikia sekta za uchumi, Aziza Mumba, alisema pamoja na kuwapo na mafanikio yatokanayo na mikopo hiyo kuna changamoto ya upungufu wa rasilimali watu wenye weledi katika kusimamia utoaji na urejeshaji wa mikopo.

Alisema kumekuwapo na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha na vitendea kazi kwa ajili ya uendeshaji wa mikopo sambamba na kuwapo kwa idadi kubwa ya maombi ya mikopo ikilinganishwa na uwezo wa halmashauri husika jambo linalopaswa kushughulikiwa.

"Ili kuondokana na changamoto hizi Kuna haja ya kila Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani ili kuongeza kiasi cha utoaji mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vinavyoomba mkopo," alisema.

Mumba,alishauri kuwapo kwa mafunzo ya uongezaji thamani ya mazao na kuunganishwa na mnyororo wa masoko kwa wanavikundi.

"Pia kuna haja ya kuwapo kwa mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ambao utasaidia kukumbusha waliokopa kurejesha fedha kwa wakati na hatimaye kuwezesha wengine kukopa."alisema

Mke wa Waziri Mkuu Mstaafu, Tunu Pinda, alitumia nafasi hiyo kueleza nafasi ya mwanamke katika uwekezaji kiuchumi na kusisitiza kuwa kutokana na wanawake wengi kuelimika na kukubali kuingia kwenye biashara hali zao za maisha zimeimarika.

Alisema usawa wa kijinsia unaoendelezwa na serikali umesaidia kwa kiasi kikubwa wanawake kujitambua na kukubali kuwezeshana wao kwa wao na kuondokana na dhana ya udhaifu iliyokuwa imezoeleka.

Pia alitumia fursa hiyo kuwashauri wanawake kuendesha biashara zao kwa kutumia mikopo kutoka taasisi za mikopo yenye riba nafuu hali itakayo wakwamua kiuchumi.



# Zanzibar yajivunia taasisi ya Karume kuzalisha wataalamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia inaendelea kuwa chimbuko la wahandisi bora nchini ili kusukuma juhudi za maendeleo.

Rais Dk. Hussein Mwinyi alisema hayo juzi kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, katika Mahafali ya Saba ya taasisi hiyo yaliyofanyika Mbweni, Zanzibar.

Alisema serikali inategemea wahitimu wa taasisi hiyo kufanya vizuri kutokana na mazingira mazuri ambayo serikali inazidi kuwaandalia ili kuendeleza uchumi wa bluu uwe wa kidigitali.

Alisema Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi hiyo katika kufanikisha ukuaji wa teknolojia Zanzibar ikizingatiwa historia ya taasisi hiyo imetoa wataalamu wengi ambao wanachangia katika maendeleo ya teknolojia kwa taifa kupitia nyanja mbalimbali. Rais Mwinyi alisema taasisi hiyo inategemewa kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha malengo na sera za nchi hususan katika maendeleo ya viwanda, sera ya uchumi wa buluu na ukuaji wa teknolojia.

Alisema dunia iko katika teknolojia na Zanzibar haipaswi kuwa nyuma na kwamba serikali imejiandaa kwenda sambamba na maendeleo hayo ambayo kuanzishwa kwa kozi mbalimbali za kiufundi na teknolojia kama kusarifu mazao ya bahari, zinatia moyo katika kufanikisha malengo ya serikali.

Dk. Mwinyi aliipongeza taasisi hiyo kwa juhudi zinazofanywa na uongozi na watendaji wake katika kuwaandaa kitaaluma na kuimarisha maisha ya vijana na kulisaidia taifa kwa kutoa wataalamu wengi wanaokidhi katika soko la ajira na kutatua changamoto za kiufundi ndani na nje ya Zanzibar.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema wizara inayoisimamia taasisi hiyo, imejipanga katika kuikuza kwa kuzidisha huduma ili kufikia azma ya serikali katika kuinua na kuzalisha wasomi wazalendo katika tasnia ya teknolojia.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi, Dk. Mahmoud Abdulwahabi Alawi, alisema wamejipanga kupitia mpango mkakati wa mwaka 2021 -2026 kuendana na kasi ya kukuza uchumi wa Zanzibar kupitia uchumi wa bluu na kwamba wataanzisha kozi mbalimbali kama vile usanifu wa mazao ya baharini.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu, Abdilahi Rashid alisema pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa kituo cha afya katika eneo hilo, hivyo kulazimika kufuata huduma hiyo masafa ya mbali na kufanya usalama wa wanafunzi kuwa tete hasa nyakati za usiku.

Wahitimu 451 wamehitimu katika mahafali kupitia masomo ya uhandisi, mawasiliano ya habari, biashara, masomo ya sayansi na hisabati pamoja na fani zingine kwa ngazi ya stashahada.




Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar Dk Mwinyi Haji Talib akifuatilia kikao cha baraza la wawakilishi kinachoendelea huko Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Udhibiti wapunguza kasi ya uvuvi haramu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu imesema kuwapo kwa maeneo ya hifadhi ya bahari Unguja na Pemba kwa kiasi kikubwa yamesaidia kudhibiti uvuvi haramu na kuimarika kwa baianuwai ya baharini ikiwemo Samaki na matumbawe.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Abdalla Juma Kombo, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu uamuzi wa serikali kutenga maeneo ya hifadhi ya baharini na faida zake katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alizitaja hifadhi hizo tano kuwa ni Chwaka na Menai yenye urefu wa kilometa 470, Kisiwa cha Mnemba (kilometa 720), Hifadhi ya Ghuba ya Tumbe Pemba (km 162.9) Changu pamoja na Bawe yenye urefu wa kilometa 900.

Pia alizitaja hifadhi zingine kuwa ni Mkondo wa Pemba ya PECCA pamoja na Misali yenye utajiri mkubwa wa hazina ya viumbe hai wakiwamo kasa.

Alizitaja faida ya kuwapo kwa maeneo ya hifadhi ni kuimarika kwa ulinzi unaotokana na doria za mara kwa mara zinazofanywa na kamati za uvuvi zilizoundwa.

Waziri alisema maeneo hayo kwa kiasi kikubwa uvuvi haramu umefanikiwa kupigwa marufuku kutokana na doria huku wavuvi wa maeneo hayo wakikubaliana kwa pamoja kufunga uvuvi wa aina ya Pweza kwa muda maalumu ili kutoa nafasi kwa viumbe hao kukuwa vizuri kabla ya kuvuliwa.

Aidha, alisema maeneo hayo yamekuwa kivutio kikubwa kwa watalii kufanya ziara za mara kwa mara kwa ajili ya kufanya utalii wa kuzamia baharini na kuangalia rasilimali za baharini na matumbawe.

# Visiwa 10 vyakodishwa kwa wawekezaji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetangaza kuwa imekodisha visiwa 10 kwa ajili ya uwekezaji na hatua hiyo itaendelea kwa awamu ya pili kwa kukodisha visiwa vingine.

Hatua hiyo ya serikali kukodisha visiwa hivyo ni kwa ajili ya kuimarisha uwekezaji na kufungua fursa zaidi kwa wawekezaji.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu ukodishwaji wa visiwa vidogo 10 vilivyotolewa kwa wawekezaji, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwekezaj Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema uwekezaji huo unaenda sambamba na Sera ya Uchumi wa Bluu inayosimamiwa na serikali na uwekezaji utafanyika kwenye bahari ambayo ni rasilimali ya Zanzibar. Alisema kampuni 53 za ndani na nje ya nchi zilionyesha nia ya kufanya uwekezaji kwenye visiwa hivyo ambavyo vilitangazwa katika awamu hiyo ya mwanzo.

Alivitaja visiwa hivyo ambavyo saba vipo Unguja na vitatu viko Pemba ambavyo ni Bawe, Changuu, Chapwani, Chumbe, Kwale, Pamunda A, Pamunda B, na visiwa vilivyoko Pemba ni Matumbini A, Misali na Njao.

Mkurugenzi huyo alisema mchakato wa kupata wawekezaji wenye uwezo ulizingatia uwezo wa mwekezaji kifedha, uwekezaji wenye tija zaidi kwa taifa (high end investment), kiwango cha mtaji wa uwekezaji, uwekezaji wenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ushirikishwaji wa wananchi na kiwango cha malipo ya awali kitakacholipwa serikali (Lease Acquisition Cost- Mahari).

Alisema kampuni zilizofanikiwa kukidhi vigezo hivyo na kubarikiwa kufanya uwekezaji kwenye visiwa hivyo ni Changuu Lodge Ltd ambayo imewekeza kisiwa cha Changuu kwa gharama ya dola milioni 20, Bawe Retreat Limited kwa Kisiwa cha Bawe kwa gharama ya dola milioni 30 na Zantexas Investment Limited kwa Kisiwa cha Chapwani kwa gharama ya Dola milioni 20.

Kampuni zingine ni Group 8 Holdings Ltd kwa kisiwa cha Kwale kwa gharama ya dola milioni 68, Chumbe Island Coral Park Limited kwa kisiwa cha Chumbe ambaye anaendelea mwekezaji wa awali na East Africa Investment Mauritius Limited kwa kisiwa cha Misali kwa gharama ya Dola milioni 83. Pia kampuni ya Tulia Zanzibar Beach Resort Limited kwa kisiwa cha Pamunda A na Pamunda B, kwa gharama ya Dola milioni 30 na kwa Pamula A dola milioni 15 na Pamula B dola milioni 15 na kampuni ya Imperial East Africa Limited kwa kiswa cha Pungume kwa gharama ya Dola milioni 10.5.

Aidha alisema Visiwa vya Matumbini na Njao havikupata wawekezaji waliokidhi vigezo, visiwa hivyo vitatangazwa tena kwenye awamu ya pili.

Sharif aliwatoa wasiwasi wananchi kuwa Visiwa hivyo havitouzwa bali vitakodishwa kwa wawekezaji hao kwa mujibu wa sheria ya Ardhi, Sheria Nambari 12 ya 1992. Aidha Serikali haikusudii kuanzisha Visiwa binafsi (Private Island) hivyo wananchi wanapaswa kuelewa kuwa uwekezaji huo hautoondoa haki zao za matumizi ya fukwe zinazozunguka visiwa hivyo wala kuondoa shughuli za kijadi, kijamii, kiuchumi na kimila zilizopo kwenye visiwa hivyo.

"Serikali inakusudiwa kuweka masharti yatakayopaswa kufuatwa na wawekezaji wote ikiwemo utoaji wa kipaumbele cha ajira kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya visiwa, uhifadhi wa mazingira na maeneo ya bahari, kutenga maeneo maalumu kwa matumizi ya wananchi ili wananchi kuendelea na shughuli zao za ukulima wa mwani, uvuvi na dago," alisema.

Alisema baada ya kukamilika kwa mafanikio makubwa awamu ya kwanza ya ukodishaji wa visiwa pamoja na kuwapo kwa mwamko mkubwa kwa wawekezaji wengi wanaotaka kuwekeza kwenye visiwa, Serikali imeamua kutangaza visiwa vingine tisa ambavyo vitano vipo Pemba na vinne vipo Unguja.

Alivitaja visiwa hivyo ni Miwi chenye ukubwa wa hekta 36.82, Popo chenye hekta 45, Fundo hekta 37, Sume hekta 3.52, Kashani hekta 31.8, Kwata hekta 6.73, Jombe hekta 76.64, Matumbini A hekta 200 na Njao hekta 470.

Alisema kuwa awamu ya pili ya ukodishwaji wa visiwa hivyo itafungua fursa zaidi za uwekezaji kinyume na awamu ya kwanza ambapo miradi yote iliyowasilishwa ni ya uwekezaji katika sekta ya hoteli.



KWELI GIGY Uk.13
UTABADILIKA?

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI

JUMAMOSI DESEMBA 25, 2021



## WAMEUPIGA MWINGI 2021

# Zuchu, Nandy pacha wanaoshindana

2021 umetajwa kuwa mwaka wa mafanikio kwa wasanii wa kike wa Bongo Fleva nchini.

Ni wazi katika kipindi hicho licha ya kuwepo na mitikisiko ya kila aina kwa baadhi ya wasanii, lakini bado walionekana kuwa imara na kujiingizia kipato kikubwa katika kazi zao.

Baadhi ya mafanikio yanayotajwa kwa wasanii wa kike mwaka huu pengine na miaka ya nyuma ni kufanikiwa kutoa albam, kumiliki mali na kuanzisha biashara zao wenyewe.

**ZUCHU**

Mwanamuziki huyu anayetoka lebo ya WCB, anatajwa kuwa kinara wa wasanii wa kike wenye mafanikio kutokana na kujiingizia pesa nyingi.

Inaelezwa Zuchu amepiga pesa nyingi kutokana na mauzo ya albam yake, matamasha ya muziki, ubalozi wa kampuni mbalimbali na biashara yake ya mavazi.

Watu wengi wanaamini mwanamuziki huyo amepata mafanikio ya haraka kuliko msanii mwingine yeyote wa Bongo Fleva.

**NANDY**

Nandy anashika nafasi ya pili katika orodha ya wanamuziki wa kike waliofanya vizuri 2021. Ndani ya mwaka huu pekee mwanamuziki huyo amejizolea kitita cha fedha kutokana na mauzo yake ya muziki, kuandaa matamasha yake ya muziki na ubalozi wa kampuni za kibiashara.

Katika moja ya sifa ambayo imewashangaza wengi ni kujiamini kwake kiasi ambacho ameamua kufanya kazi yeye mwenyewe na bila kushirikisha watu wa kati.

**GIGY MONEY**

Pamoja na kuonekana mtukutu, Gigy Money, inaaminika amepata pesa nyingi mwaka huu kutokana na kuwa balozi wa kampuni tofauti za kibiashara.

Mwaka huu aliuanza vibaya baada ya kufungiwa na serikali kujishughulisha na muziki, lakini bado aliendelea kupata umaarufu na hata alipofunguliwa bado alipiga pesa.

BASI SAWA

## Shilole ataka wanawake kukataa mateso 2022



MWANAMUZIKI na mjasiriamali, Shilole, ametoa ushauri wake wa kumaliza mwaka 2021, akiwataka wanawake wanaonyanyasika kujitafakari na kama wakiona wanaelemewa na mateso kujiondoa katika ndoa.

Akizungumzia mgogoro uliopo kati ya msanii Shaa na prodyuza mkongwe Master J, amesema kwamba katika ndoa kuna kikomo cha uvumilivu na kinachofuata hapo ni maumivu na wakati mwingine kifo.

"Unaweza kuvumilia kumbe unakiita kifo, ushauri wangu kama Shaa kashindwa ni bora kuchukua hatua ya kuondoka na nawasihi wanaume waache manyanyaso kwani mwanamke anahitaji matunzo na kubembelezwa," amesema.

## Marioo ajipongeza 2021



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Marioo amesema mwaka 2021 una mafanikio kwake kutokana na kufanya vizuri katika kazi zake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Marioo amesema kama ingekuwa tuzo angepata katika vipengele vitano muhimu kutokana na nyimbo zake kuwa na vigezo muhimu.

"Niseme asante kwa mwaka huu kusema kweli nimeupiga mwingi sana, tungekuwa na tuzo zangu zingekuwa tano," amesema.




## Lulu Diva wengi wamtetea

MENGI yamesemwa kuhusu Lulu Diva baada ya mazishi ya mama yake yaliyofanyika mkoani Tanga

Lakini suala la nyumba ya udongo waliyofikia wafiwa na waombolezaji imeibua mjadala kinzani, kuna wale wanaomlaumu kwa kutojenga nyumba ya kisasa kijijini kwake na wapo wanaomtetea kuwa hilo si jukumu lake. Mmoja wa wanaosimama kumtetea Lulu Diva ni Roma Mkatoliki, ambaye katika ujumbe wake wa Twitter amesema watu wakija mjini kila mtu ana mipango yake na hivyo mengine hayawahusu.

"Haya mambo ya kwanini hujajenga kwenu, sijui muoneni ana-ball tu town ila kwao hajajenga hayawahusu, town kila mtu ana mipango yake bana". Amesema



## Kweli Gigy utabadilika?

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva na muigizaji, Gigy Money, amejitabiria mwaka 2022 utakuwa tofauti kwake kuanzia mwonekano na vitendo.

Gigy ambaye ni mama wa mtoto mmoja Mayra, amesema amechoka kuonekana kama mwanamke chakaramu na baadhi ya watu wanavyomchukulia, hivyo anataka kubadili mtizamo huo.

"Maisha ni vile unaamua kuishi, ukitaka kuonekana serious au miyeyusho is all on you baby, binafsi nimechoka kuonekana miyeyusho niko serious kuliko akili yako inavyofanya kazi". Amesema.




## Wakati Ukuta: Lenye sura lina kisogo

**Na Adam Fungamwango**

HUU ni msemo maarufu sana Tanzania 'Jogoo la Shamba haliwiki mjini.' Waswahili wana maana kuwa mtu yoyote anayetoka kijijini ni lazima atapata changamoto kubwa anapofika mjini kutokana na mazingira anayokutana nayo ambayo ni tofauti na kule alikotoka.

Wa kijijini ni lazima atashangaa vitu vingi ambavyo vitakuwa vipya kwake na vingine hatoweza kuvitumia bila msaada wa mwenyeji.

Lakini kwenye filamu hii ya 'Wakati Ukuta' imekuwa ni tofauti kidogo. Hii sasa ni jogoo wa mjini aliyekwenda kuwika shamba. Akawika hasa, lakini kilichomkuta huko huyo jogoo ni kuchinjwa tu. Inshu kwenye filamu hii iliyochezwa na kina Luckey Luckano aliyecheza kama Paschal na Stanley Msungu iko hivi.

Paschal mtoto wa mjini anayeishi na dada yake, ni kijana mtanashati, lakini hajatulia. Ana tabia ya kutembea na wasichana hovyo, hadi wengine kuwazalisha.

Tabia hiyo inamkera sana dada yake, lakini hana la kufanya na kumfukuza hawezi.

Kuna ndugu yao anafariki huko kijijini. Wote wawili wanakwenda kwenye msiba. Lakini unapomalizika, dada mtu anamwambia Paschal kwanza akae hapo japo kwa mwezi mmoja ili kuzuia uwezekano wa baadhi ya ndugu zao kujimilikisha nyumba hiyo pamoja na mashamba ambayo hayawahusu kwenye urithi. Paschal anakubali. Shughuli ndipo inapoanzia.

Utanashati wake unawaduwaza na kuwapumbaza wasichana wengi kijijini na wengine wake za watu. Kama kawaida yake, Paschal ni samaki asiyepisha chambo. Anaanza kutembea na kila msichana anayejipitisha na kujipendezesha kwake. Lakini mwenyewe rohoni mwake alimpenda msichana mmoja anayeitwa Doroth. Doroth naye akampenda Paschal. Msichana kazi kwao zikawa hazifanyiki. Kutwa kiguu na njia kwa Paschal, kiasi cha mama yake akaanza kuhisi kuna kitu.

Kelele za mama yake Doroth zilimfanya binti amsihi mpenzi wake ajitambulishe kwao, kwani mambo ya kuibana yanasabisha wasilifaidi penzi. Lakini kwa sababu Paschal hakuwa muoaji, bali ni mfujaji, alikuwa akimdanganya tu ipo siku atajitambulisha tu.

Siku zilipokuwa zikizidi kusonga mbele, kijana huyo alinuka. Tetesi zikawa kubwa kuwa mbali na kuwa anatembea na vibinti vidogo, lakini pia anatembea na wake za watu. Mtego ukawekwa. Siku hiyo Paschal akabambwa anatembea na mke wa Msungu. Kelele kama za mwizi zikapigwa, kila mkazi kijijini hapo akatoka na silaha. Bila kumuangalia mtu usoni, mhalifu akapigwa hadi kufa.



## Ya Gigy yaache yapite

**Na Adam Fungamwango**

WASANII wana uwezo mkubwa wa kuigiza kwenye baadhi ya maeneo kwa ustadi zaidi kuliko sehemu nyingine. Kuna wanaoweza kuigiza kucheza uswahilini, hasa wale wenye uwezo wa kusuta, na maneno ya shombo, mbwembwe na tashtiti.

Wapo wenye uwezo wa kuigiza mabosi, matajiri na hata kuigiza baba mkali. Siyo kwamba wengine hawawezi, ila kuna wenye uwezo wa kuigiza kwa ustadi zaidi.

Leo tutawaangalia wasanii ambao wakicheza maeneo ya vijijini wanaonekana kucheza kwa ustadi zaidi kuliko eneo lingine.

**MOHAMED FUNGAFUNGA 'MZEE JENGUA'**

Pamoja na kwamba kuna wakati hucheza maeneo ya mjini, lakini ukitaka umfaidi zaidi acheze kama mkazi wa bushi.

Anajulikana kama ni mzee mtata, mkorofi, mkoloni, asiyetaka ushauri au kumsikiliza mtu yoyote kwa kile ambacho yeye anakiamini, kiwe kizuri au kibaya.

Akicheza shamba, wakati mwingine huwa kama mfalme, mtemi, baba, mwanakijiji au mchawi, huteka mashabiki wengi kutokana na aina yake ya uigizaji wa ukali uliopitiliza. Alifariki dunia Desemba mwaka jana.

**FADHILI MSISILI 'MSISILI WA MSISILI'**

Ni mmoja kati ya wazee wenye uwezo mkubwa wa kuigiza hasa akiigiza akiwa kijijini.

Utampenda zaidi akiigiza kama mfalme au mtemi, lakini pia wakati mwingine huigiza kama mzee wa kijiji mwenye busara au baba wa familia.

Mzee Msisili ana pande zote mbili. Anaweza kuigiza ukali au ukatili kama akiwa mtemi, lakini anaonekana kuwa na hekima na busara kama akiwa mzee wa kijiji au baba wa familia.

Mashabiki wengi wa filamu huwa hawapendi kumuona mzee huyu akipewa 'sini' za mjini.

**FATUMA MAKONGORO 'BI MWENDA'**

Wengi wanamfahamu mama huyu kuwa ni mkorofi na mchawi. Ni kwa sababu watengenezaji wengi wa filamu wanaona anafaa sana kuigiza sehemu hizo na anavyoigiza analeta uhalisia zaidi.

Pamoja na yote hayo, Bi Mwenda anapendeza zaidi akiigiza 'uchawi' wake akiwa kijijini zaidi kuliko mjini.

Na hata akiigiza kwenye 'sini' nyingine kama vile mama wa familia, utampenda zaidi akiwa kwenye mazingira ya bushi.

**HAMISI KORONGO 'MZEE KORONGO'**

Kwenye tasnia ya filamu kumezuka baadhi ya wasanii wenye umri mkubwa wenye uwezo wa hali ya juu, kiasi cha wengine kujiuliza walikuwa wapi siku zote.

Mmoja wapo ni huyu mzee Korongo. Ni mzee mwenye kipaji cha hali ya juu kwenye uigizaji.

Anafiti kucheza maeneo yote ya mjini na kijijini, lakini ili umfaidi na kuona uwezo wake, basi awekwe kwenye 'sini' za kijijini, utampenda.

**ALLY NOGI**

Huyu mzee utampenda sana ukiangalia filamu moja inaitwa 'Najua Kuoa'. Amecheza na Riyama Ally.

Hii ni filamu maarufu sana na hata wale waliokuwa hawamfahamu msanii huyu, wameanza kumfahamu na kumfuatilia baada ya kuitazama hiyo.

Alicheza kama baba wa kijijini na mkewe Riyama, marehemu Mzee Majuto na wengineo.

Kutokana na kuicheza filamu hiyo kwa ustadi wa hali ya juu, hata wanaompa kazi nyingine ya kucheza filamu mara nyingi humtafutia mazingira yale yale ya kijijini ili kuufaidi uwezo wake Mzee Ally Nogi.



BI MWENDA



# Warembo hawa wametisha 2021

WAREMBO wanaotawala katika mitandao ya kijamii Nance Isime na Saskay wametajwa kuongoza katika orodha ya mastaa wanawake waliofanya vizuri 2021.

Kulingana na mtandao wa Pulse, Nance ameshika nafasi ya kwanza na Saskay amemfuata kwa karibu katika utafiti uliofanywa.

Nafasi ya tatu imechukuliwa na nyota wa vipindi vya televisheni, Maria , huku mwanamuziki Tiwa Savage akishikilia nafasi ya nne.

Namba tano imeshikiliwa na Tems, kisha wakifuatia Yemi Alade,Toke Makinwa na Tacha.



## Wizkid amzawadia SUV meneja wake

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Wizkid amefanya jambo la kiungwana kwa meneja wake baada ya kumzawadia gari la kifahari aina ya Toyota Land Cruiser SUV.

Kupitia ukurasa wa Instagram, msanii huyo aliweka picha tofauti akionyesha kumkabidhi gari hilo meneja wake kama shukurani zake kwa kazi anazomfanyia.

Hii sio zawadi yake ya kwanza kuwapa watu wake wa karibu, mwaka jana alifanya hivyo kwa timu yake kwa kuwazawadia magari.

## Karibi afariki dunia

MSANII mkongwe wa filamu za Nollywood, Karibi Fubara amefariki dunia.

Kifo hicho kimetangazwa na dada yake Aya Eneli, kupitia ukurasa wake wa Twitter siku ya jumanne.

"Kaka yangu kipenzi Karibi Fubara, ameungana na malaika mbinguni, nimevunjika moyo si kwa kuondokewa matumaini, ameondoka kimwili lakini kiroho yupo pamoja nasi," amesema.





## Maraji naye kuwa mama

MSANII wa vichekesho kutoka Nigeria, Gloria Olorunto maarufu kama Maraji, hatimaye amepata ujauzito.

Maraji kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliweka video fupi akionekana akiwa amevaa nguo maalumu inayovaliwa na wanawake wajawazito.

Muda mfupi baada ya kuwekwa, mashabiki wake waliuteka ukurasa huo kwa kila mmoja akimtakia heri ya kuwa katika hali hiyo.

## Ben acha wakukumbushe kidogo

MWIGIZAJI wa filamu kutoka Hollywood, Ben Affleck amekuja juu baada ya kukumbushwa mkewe wa zamani Jennifer Garner.

Katika kipindi cha mahojiano cha Jimmy Kimmel, mkongwe huyo wa filamu alionekana kutokuwa tayari kuelezea uhusiano wake na aliyekuwa mkewe huyo na kusema hawezi kusema chochote kwa sababu jambo hilo limepita.

"Tumesema kuhusu familia yangu, talaka na unywaji wa pombe na kwamba hatuwezi kuhesabu chochote kuhusu mapenzi," amesema.



MAKALA

# EMMANUEL THEONEST KATO

## ●Mwanafunzi bora aliyezoa tuzo tano
## ●Kinara wa utafiti Chuo Kikuu Ardhi

**Na Joseph Mwendapole**

Emmanuel Theonest Kato ni mwanafunzi aliyemaliza Chuo Kikuu Ardhi (ARU) mwaka huu akiwa amepata ufaulu mkubwa kuliko wengine wote hivyo kupewa zawadi ya mwanafunzi bora.

Emmanuel alisomea Shahada ya Sayansi ya Mazingira na Usimamizi, alijiunga na ARU mwaka 2017 na kufanikiwa kupata GPA ya jumla alama 4.6 iliyomfanya kuchaguliwa kuwa mwanafunzi bora wa kiume kwa mwaka wa masomo 2020/2021.

Anataja siri ya mafanikio katika safari nzima ya masomo yake chuoni hapo kuwa ni kumtanguliza Mungu, kuweka juhudi, nidhamu kuhudhuria darasani na kusoma kwa bidii kwamba hayo yaliweka misingi imara katika safari ya masomo ya chuo kikuu tangu alipoingia mwaka wa kwanza mwaka 2017.

"Kilichonifanya nichague fani hii ya mazingira nadhani ni mpango wa Mungu maana nilifanikiwa kupata udahili katika vyuo viwili wakati wa kutuma maombi ya kuomba chuo ambavyo ni MUST Mbeya nilichaguliwa Civil Engineering na ARU nikachaguliwa Sayansi ya Mazingira na Usimamizi," anasema Emmanuel ambaye ni mtoto wa tatu kati ya watoto wanne wa mzee Kato.

Anasema baada ya kutafakari kwa kina pamoja na wazazi wake, aliona ni vyema akasome sayansi ya mazingira kwa sababu kuu mbili akitaja ya kwanza kuwa ni mazingira ni vitu vyote vinavyomzunguka binadamu.

"Niliona mazingira kama jambo ambalo linapewa kipaumbele sana hasa katika nchi yetu utunzaji wa mazingira ni swala la muhimu sana ambalo linahitaji kupewa kipaumbele kwani linachangia katika uhai wa binadamu, maana uharibifu ukitokea katika mazingira basi tunayataharisha pia maisha ya viumbe hai pamoja na sisi wanadamu," anasema.

Anasema uchafuzi na uharibifu wa mazingira yetu yanachangiwa kwa asilimia kubwa na binadamu ambao licha ya kupata vitu vyote kutoka kwenye mazingira, lakini wanaongoza kwa kuyaharibu.

Anaeleza kwamba wananchi wanapaswa kushirikiana katika kutunza mazingira kama urithi wa kipekee waliopewa na Mungu.

"Hili jambo lilinivutia sana na kama nilivyosema awali kwa mpango wa Mungu nikafanikiwa kuchaguliwa kusoma elimu ya juu Chuo Kikuu Ardhi kozi ya sayansi ya mazingira na usimamizi.

"Natamani siku moja kuwa mdau au nafasi moja serikalini mwenye dhamana ya kutunza na kulinda mazingira ambaye ataleta chachu katika maswala ya kutunza mazingira yetu" ameongeza kusema.

Anaeleza mazingira yanategemea maswala yote ya mabadiliko ya tabia ya nchi, uchafuzi wa vyanzo vya maji na matatizo mengine kimaumbile.

Anasema kwa wanafunzi ambao wanatamani kufikia ufaulu mzuri katika masomo yao, amewataka kutokata tamaa hata mara moja kwani nidhamu, juhudi na kujitambua ni mambo ya msingi katika kuelekea mafanikio.

"Lakini yote wasimsahau Mungu kamwe maana bila nguvu zake sisi hatuwezi chochote.Napenda kuwaaasa kuwa wakiyashika hayo yote basi watumainie mafanikio mbele yao sio katika masomo yao tu, bali hata katika safari nzima ya maisha hapa duniani," anaasa.

Kutokana na ufaulu mzuri aliopata Emmanuel Kato, alipata zawadi tano ambazo ni mwanafunzi bora katika Idara ya Sayansi ya mazingira na usimamizi mwaka wa nne na mwanafunzi bora kwa ujumla katika shule ya sayansi ya mazingira na teknolojia kwa mwaka 2020/2021.

Nyingine ni mwanafunzi bora mvulana Chuo Kikuu Ardhi mwaka 2020/2021, mwanafunzi bora wa mwaka wa nne katika utafiti (dissertation) katika Shule ya Sayansi ya Mazingira na Teknolojia na mwanafunzi bora kwa ujumla Chuo Kikuu Ardhi katika mwaka.

"Awali yote nipende kuchukua nafasi hii kushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Ardhi pamoja na walimu wote kwa ujumla kwani wamefanya kazi kubwa katika kutupa elimu ambayo ni ya msingi sana katika safari yetu ya maisha," anasema.

Ameshukuru uongozi wa Shule ya Sayansi ya Mazingira na Teknolojia pamoja na walimu wote wa shule ya Sayansi ya Mazingira na Usimamizi kwa kutoa muda wao kuwafundisha, kutoa ushauri na kuwapenda kama watoto wao kwa muda wote chuoni.

Pia atoa shukurani zake kwa walimu wake waliomsimamia katika utafiti wa kumaliza chuo ambapo ambapo alikuwa anaangalia athari za kiekolojia za microplastics kwenye samaki wa mto Kibangu jijini Dar es salaam ambao ni Dk. Muhondwa na Chrisogoni.

Anasema walimu hao wamemuongoza na kumsimamia salama hadi utafiti ulipokamilika zaidi na pia aliwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika safari yake ya masomo chuo Kikuu Ardhi.

Emmanuel mwenye kaka wawili na mdogo wake wa kike mmoja, anawashukuru wazazi wake Kato Kabaka ambaye ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji jotoardhi Tanzania na Mama yake Dorosela Bonabana Tibagilwage kwa malezi bora waliyomlea.

Anasema mpaka leo hii alipofikia wamehangaika kwa ajili yake kwa nguvu, juhudi na pasipo kuchoka wamejaribu kujitoa kwa kadri ya uwezo wao kumsaidia pia wamechangia kwa kiasi kikubwa katika safari ya masomo na maisha yake.

"Kiujumla namuomba Mungu awabariki na awazidishe pale walipopunguza na nawapenda sana na naahidi kuwa nitaendelea kuwa mwaminifu na mtoto bora wa mfano kwao kwa watu wengine katika jamii kama ili wavijunie mtoto wao kama wanavyotamani siku moja niwe," anasema .



Emmanuel Kato

**"Niliona mazingira kama jambo ambalo linapewa kipaumbele sana hasa katika nchi yetu utunzaji wa mazingira ni swala la muhimu sana ambalo linahitaji kupewa kipaumbele kwani linachangia katika uhai wa binadamu, maana uharibifu ukitokea katika mazingira basi tunayahatarisha pia maisha ya viumbe hai pamoja na sisi wanadamu," anasema.**

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Vibweka vya wenye TV zilipoingia Bongo



Na Adam Fungamwango

ILIKUWA ni patashika nguo kuchanika, kwa kinamama na watoto ambao hawakuwa na televisheni wala video katikati ya miaka ya 1990 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Baadhi yao walipata tabu sana, wa kikumbwa na masharti mbalimbali ya kushangaza, kuchekesha wanapoenda kutaka kuangalia tamthilia mbalimbali iliyokuwa ikionyeshwa na ITV, iliyokuwa ikichezwa na wasanii wa Kitanzania waliokuwa kwenye makundi ya sanaa kama Kaole, Kidede na Mambo Haya.

Tamthilia ya nje ambayo ITV ilikuwa ikionyesha ni ya Tausi, ikiwa na wasanii maarufu sana wakati huo kama kina Ashina Kibibi au Siti Binti Kasri, Mjuba, Lindi, Chokoraa Damu, Karumanzira na wengineo.

Ikumbukwe kuwa, miaka hiyo TV zilikuwa ndiyo kwanza zinaingia nchini, kama ilivyokuwa simu za mkononi, hivyo ni watu wachache sana waliokuwa nazo.

Mtaa mzima anaweza akawapo mtu mmoja. Wakati mwingine hata mitaa sita, kijiji au kitongoji kizima kukawa na watu wawili au mmoja tu mwenye TV.

Hapo sasa upate mtu mwenye moyo au roho ya huruma na upendo, vinginevyo ama wanaokwenda kuangalia watatimuliwa, au kukutana na masharti magumu.

Nimesema hapo juu kuwa mara nyingi kinamama na watoto ambao wengi hawakuwa na TV, ndiyo waliokuwa wakitoka majumbani kwao kuelekea kule ambako kuna nyumba zenye TV.

Kwanza kabisa watoto waliambiwa kuwa wasije kuangalia TV kama hawajaoga. Hilo ni sharti la kwanza na hata wakati wa kuingia watoto hukaguliwa kama wanaingia kwenye kambi ya jeshi.

La pili, ni kwamba hakuna kuingia na viatu ndani. Pia watoto hawakutakiwa kukaa kwenye makochi, ni chini, vilevile hakuna mtu kugusa ukutani, ukifumwa tu inaweza ikawa ndiyo tiketi yako ya kutolewa nje.

Sharti lingine ni kutopiga kelele. Kitendo chochote cha mtoto yoyote kupiga kelele kiliweza kusababisha TV kuzimwa na kila mmoja kuondoka nyumbani kwake.

Siku za wikiendi, na masaa machache kabla ya mchezo, akinamama walikuwa wakipika mapema ili mradi tu kupata muda wa kwenda kuangalia michezo na watoto wao.

Wazee waliokuwa na TV wakawa maarufu sana mitaani na vijijini.

Jamaa mmoja alisema kuwa kijijini kwao kulikuwa na mtu mmoja tu ambaye alikuwa na televisheni, hivyo watu wazima, wake kwa waume na watoto walikuwa kila siku jioni wakimiminika nyumbani kwake kwenda kuangalia vipindi mbalimbali, hasa michezo ya kuigiza na tamthilia, lakini baadaye akawageuza fursa.

Kipindi cha mavuno ya mahindi wakawa wanayamwaga sebuleni, sasa wale wote waliokuja kuangalia TV ikawa kazi kwao kuyapukuchua. Unapukuchua huku unaangalia TV.

Mwingine anasema kuwa wao karibuni mtaa mzima walikuwa wakienda kuangalia kwa mzee fulani mtaani kwao, kwa kweli anasema mzee yule alivumilia sana, maana nyumbani kwake kulikuwa kunajaa sana watu hadi wakawa wanafikiria namna ya

**Jamaa mmoja alisema kuwa kijijini kwao kulikuwa na mtu mmoja tu ambaye alikuwa na televisheni, hivyo watu wazima, wake kwa waume na watoto walikuwa kila siku jioni wakimiminika nyumbani kwake kwenda kuangalia vipindi mbalimbali, hasa michezo ya kuigiza na tamthilia, lakini baadaye akawageuza fursa**

kula, maana watu wamejazana kuanzia uwanjani kwake hadi sebuleni ambako TV ipo.

Ilikuwa ni shida sana kwa watoto ambao nyumbani kwao hakukuwa na TV, kwani ukimchokoza mtoto ambaye kwao wanayo, basi wala si ajabu ukaambiwa usiende kwao kuangalia, na iwe bahati nzuri mtaani kuwe na watu angalau wawili au watatu wanayo, lakini kama ni huyo huyo tu, basi huangalii kweli.

Nakumbuka kuna mzee mmoja mitaa ya Mwananyamala kwa Kopa, yeye alikuwa na TV, na kwa kuwa alishawazoesha watu kila Jumamosi na Jumapili wanakuja kuangalia tamthilia, basi hata kama yeye na mkewe hawapo, watawaachia maagizo watoto wao jinsi gani ya kuiwasha TV na kuizima ili watu wakija wasikose kuangalia.



Kutokana na hilo, wakazi wa maeneo hayo walikuwa na uhakika wa kutazama tamthilia hata kama yeye na mkewe hawapo. Ilikuwa ni majozi na huzuni tele kwa wakazi wa eneo lote lile alipohama na kuhamia kwenye nyumba yake aliyojenga maeneo ya Madale.

Sasa usiombe ukutane na wale ambao wao hawataki kabisa watu waende kuangalia kwao. Kwanza, tumeona wale ambao wanaruhusu, lakini kwa watoto masharti yanakuwa kibao, pili kwa watu ambao hawana matatizo, sasa kwa wale ambao ni watata.

Hawa ni wale waliokuwa wanaangalia wao na familia zao tu. Hapa sasa watoto wa jirani watakuwa wanafanya kazi ya kunyemelea kwenye madirisha. Watoto wataumwa na mbu hapo balaa na wakati mwingine hata kutimuliwa na mwenyewe kwa matusi, viboko na kashfa.

Hii ilisababisha wazazi wengi kuingiwa na uchungu na kujinyima ili wawanunulie watoto wao TV, kutokana na manyanyaso wanayoyapata kwa wale ambao hawakuwa na huruma na watoto wa jirani zao.

Yupo mmoja aliniambia baba yao alikuwa bahili sana, lakini alilazimika kesho yake asubuhi tu kwenda mjini kununua TV na deki, baada ya mkewe, yeye na mdogo wao kumwagiwa maji, walipoenda kuangalia tamthilia kwenye nyumba ya jirani.

Waliporudi mapema, huku wakiwa wamelowa na kuwauliza kulikoni, alipoambiwa hivyo alipatwa na uchungu, kesho yake akaamua kuweka ubahili pembeni na kwenda kununua kwa ajili ya familia yake.

Ukiachilia mbali hilo, kuingia kwa televisheni nchini, kulisababisha kuibuka kwa wimbi la wizi wa kumi nje , kumi ndani, pamoja na jiwe lililopewa jina la 'fatuma'.

Aina hii ya wizi ilitumika wa wezi kwenda kuiba TV sehemu ambazo tayari zimeshathibitika kuwa zipo.

Linakuja lundo la wezi ambao hata kama hawafiki 10, watawatishia watu, kwa sauti kuu, 'kumi nje kumi ndani', lango linavunjwa na jiwe kubwa maarufu Fatuma, watu wanabeba TV na kuondoka nayo, tofauti na sasa ambapo hata akionekana mtoto ameibeba mtaani, watu hata habari naye hawana.

Wizi huu ulisababisha TV nyingi kujengewa kwa kuzungushiwa nondo, au kabati ambalo linafungwa na funguo anakuwa nayo baba tu, au usiku watu wakitazama inaingizwa chumbani kabisa na kufichwa. Tofauti na sasa ambapo TV inalala sebuleni.

**Tuma sms: 0716 350534**

# UAE yasitisha usafiri wa ndege mataifa matatu A/Mashariki

**DUBAI,** UMOJA WA FALME ZA KIARABU

UMOJA wa Falme za Kiarabu (UAE), umetangaza kusitisha safari za ndege kwa abiria kutoka Tanzania, Kenya, Ethiopia, na Nigeria na kuongeza vikwazo vya usafiri kwa ndege za Uganda na Ghana, kuanzia Desemba 25, mwaka huu.

Mamlaka ya Kitaifa ya Kudhibiti Dharura na Majanga (NCEMA) na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (GCAA) za nchi hiyo zimesema hatua hizo mpya zitaanza kutekelezwa kuanzia saa moja na nusu usiku wa Jumamosi.

Hatua hiyo inajumuisha kusimamisha kuingia nchini humo kwa wasafiri waliokuwa katika nchi hizo nne siku 14 kabla ya kusafiri UAE. Hata hivyo safari za ndege kutoka UAE hadi nchi hizo zinaendelea kama zilivyoratibiwa.

Nchi hiyo pia imeweka masharti mapya ya usafiri kwa abiria wanaokuja kwa ndege za moja kwa moja kutoka Uganda na Ghana.

Masharti hayo ni pamoja na kufanyiwa vipimo vya COVID-19 ndani ya saa 48 na kufanyiwa vipimo vya-PCR kwenye uwanja wa ndege ndani ya saa sita kabla ya kuanza safari.

Raia wa UAE wamezuiwa kusafiri kwenda nchi hizo nne za Kiafrika isipokuwa kwa matibabu ya dharura, ujumbe rasmi na ufadhili wa masomo.

Wale walioondolewa kwenye marufuku ya usafiri lazima wawasilishe vipimo hasi vya PCR ndani ya saa 48 baada ya muda wao wa kuondoka, wakapime haraka PCR kwenye uwanja wa ndege saa sita kabla ya kuondoka, na wafanyiwe tena vipimo watakapowasili UAE.

Hivi karibu Tanzania ilizindua mashine nyingine kubwa na ya kisasa kwa ajili ya kupima kipimo cha haraka cha Covid -19 kwa wasafiri wanaoenda nchi hiyo, baada ya kuwataka wasafiri wanaotokea Tanzania kwenda Dubai, kupata vipimo vya masaa 48 na kisha kumalizia na kipimo cha saa sita kabla ya safari.

**BBC**



Wanajeshi wa Ethiopia wakipiga doria kwenye mji wa Dessie katika jimbo la Amhara walioutwaa kutoka vikosi vya TPLF. (**PICHA: DW**)

# Ethiopia yaamuru vikosi vyake kubaki ndani ya uwanja wa vita

**ADIS ABABA,** ETHIOPIA

SERIKALI ya Ethiopia imewaamuru wanajeshi wote walio kwenye uwanja wa mapambano kubaki kwenye maeneo waliyoyakomboa kutoka kwa wapiganaji wa Jeshi la Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPLF).

Hata hivyo, mkuu wa kitengo cha mawasiliano ya serikali ya Ethiopia, Legesse Tulu, alisema vikosi hivyo havitaingia ndani zaidi ya jimbo la Tigray..

Jeshi la shirikisho la Ethiopia na washirika wake wamepata mafanikio ndani ya wiki za hivi karibuni, wakikomboa miji mikubwa na midogo katika mikoa jirani ya Amhara na Afar, ambayo wapiganaji wa Tigray walikuwa wameitwaa mapema mwaka huu.

"Awamu ya opereshani ya kuliondosha kundi la kigaidi kutoka kwenye maeneo liliyoyavamia imekamilika kwa ushindi. Kwa sasa, hamu na uwezo wa adui kupambana umeharibiwa vibaya vibaya," alisema Legesse.

Aliongeza "Serikali itachukuwa hatua zaidi kuhakikisha kwamba vikosi vya Tigray havingii tena siku zijazo. Kwa sasa, wanajeshi wa Ethiopia wanaamriwa kushikillia maeneo ambayo tayari wanayadhibiti,"

Tangazo hilo la serikali ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed ,kwamba wanajeshi wake hawatapambana tena na vikosi vya Tigray ndani ya jimbo lao inaweza kuwa hatua mpya inayoonyesha usitishwaji mapigano na mazungumzo ya kuutatua mzozo huo.

Ushindi huo unatokana na jeshi la Ethiopia kuimarika kutokana na ndege zisizo rubani zilizonunuliwa China, Uturuki na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Mapema wiki hii, Mkuu wa vikosi vya Tigray, alisema wapiganaji wake wameamriwa kujiondoa kwenye maeneo waliyokuwa wakiyashikilia na kurejea jimboni. Alipendekeza kuwepo kwa eneo lisiloruhusiwa ndege kuruka ili kuzuia mashambulizi kutoka angani kwenye mkoa wake na kuwekwa kwa vikwazo vya silaha dhidi ya Ethiopia na Eritrea.

Makumi kwa maelfu ya watu wameuawa katika mzozo huo wa Tigray uliozuka mwezi Novemba 2020, kati ya vikosi vya serikali ya Ethiopia na wapiganaji kutoka jimbo la Tigray, waliokuwa na nafasi za juu kwenye serikali ya Ethiopia kabla ya Abiy kuingia madarakani mwaka 2018.

**DW**

## X-Mass yagubikwa na hofu ya Omicron

**BETHELEM,** ISRAEL

MAMILIONI ya waumini wa dini ya Kikristo duniani wanasherehekea Sikukuu ya Krismasi kwa mara nyingine zitagubikwa na kiwingu cha janga la virusi vya corona.

Ibada ya mkesha wa sikukuu hiyo inayosherehekea kuzaliwa kwa Yesu Kristo zilifanyika usiku wa leo na kuendelea katika wakati ambapo mataifa mengi duniani yamerejesha vizuizi vikali vya kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Mjini Bethelem, eneo linaloaminika kuwa Yesu Kristo alizaliwa zaidi ya miaka 2,000 iliyopita, watalii hawataweza kulifikia baada ya Israel kuifunga tena mipaka yake kwa hofu ya kuenea kwa kirusi kipya cha corona, Omicron.

Barani Ulaya, mataifa kadhaa ikiwemo Ujerumani, Uholanzi, Italia, Ufaransa na Uhispania yametangaza masharti fulani yanayozuia mikusanyiko ikiwa ni pamoja na ruhusa ya watu waliopatiwa chanjo kualika wageni wachache kwa ajili ya sikukuu hiyo.

**DW**

## Watuhumiwa wa ugaidi kortini

**KAMPALA,** UGANDA

UGANDA imewafungulia mashtaka ya ugaidi watu 15 akiwemo mwanamke mmoja mjamzito kwa tuhuma za kuhusika na mashambulizi ya mabomu ya hivi karibuni.

Naibu Msemaji wa Polisi ya Mji Mkuu, Luke Owoyesigyire, alisema watuhumiwa hao walipandishwa kizimbani juzi kujibu tuhuma za ugaidi na kuwa wanachama wa kundi la itikadi kali. Ofisa huyo wa polisi, alisema watuhumiwa hao wanahusishwa na mashambulizi manne ya mabomu mjini Kampala ya mwezi Oktoba na Novemba, na watasalia kizuizini hadi kesi yao itakapotajwa tena Januari 13.

Uganda ilidai mashambulizi hayo ya mabomu yalipangwa na kundi dogo la kigaidi nchini humo lenye mafungamano na kundi la waasi la ADF ambalo Marekani inadai lina uhusiano na kundi linalojiita Dola la Kiislam.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KIWANJA KIANUZWA.

KIWANJA KIANUZWA KISUSURU JKT KIWANJA KIPO KISUSURU JKT SEGEREA UKUBWA SQM 2252 KINA HATI BEI MILIONI 55, **KWA MAWASILIANO: 0786 857523 AU 0655 857523**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZUHURA AWADHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha **KUHITIMU MAFUNZO UALIMU** chenye registration namba **E.507-0214** kilichotolewa kupitia chuo cha **MOROGORO TEACHER TRAINING COLLEGE(MOROGORO TTC)** mwaka 1992,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **TAN/TAN/RB/599077/2021**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MATANGA MAPUNDA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0720-0039** kilichotolewa na baraza kupitia shule ya secondary ya **MPITIMBI mwaka 2004,**na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0882-0588** kilichotolewa na baraza kupitia shule ya secondary ya **SONGEA MUSLIM SEMINARY mwaka 2008 n**a cheti cha diploma kozi ya **DIPLOMA IN SECONDARY SCHOOL chuo cha SONGEA TEACHER'S COLLEGE** chenye namba E0509-422 kilichotolewa mwaka 2010
Polisi taarifa **SO/RB/7932-2017**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**Probate and administration**
**cause no.206 of 2021**

**IN THE MATTER OF THE STATE OF THE LATE ANDREA MOSES MSATI AND**

**In the matter of application letter of administration by MICHAEL ANDREA MSATI**

**GENERAL CITATION**
**(rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration)is made to the above named petitioner
Objections to the grant should be filed on before the 7th day of January,2021
Dated at dar es salaam this 13th day of desember,2021

## KUPOTEA KADI YA GARI

**LOTTA MARSELIN NKONDORA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SCANIA** yenye namba za usajili **T 885 CCK,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa MKB/RB/3705/2021**

## KUPOTEA KADI YA BAJAJ

**KELVIN STIVIN MTENDE ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **BAJAJ** yenye namba za usajili **MC 327 CLM** Injini namba **AK4NK4306091** chasiss namba **MD6M14PAOK4N05819** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/MUF/RB/462471/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI MADOGO NA: 121/ 2020.**

**JONATHAN KAGARUKI..............................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1.HASSAN HUSSEIN**
**2.HARUNA HUSSEIN..................WAJIBU MAOMBI**

**KWA:HASSAN HUSSEIN NA HARUNA HUSSEIN**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi madogo Na.121/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 31/01/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R.Mtei saa2:00 Asubuhi.
Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/ mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.
AMRI. Hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 07/11/2021.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

**IN THE DISTRICT COURT OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**
**CIVIL CASE NO 5 OF 2021**
**GESAP ENGINEERING GROUP LTD............................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**1.SONIA ENTERPRISES COMPANY LTD.........DEFENDANT**
**2.MAHAMUD HAJI SWAHIBU.......................................DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**
**TO:MAHAMUD HAJI SWAHIBU**

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for Mention on the 30 th day of **DECEMBER, 2021 at 8:30 O'clock** in the forenoon,Before **HON A.W.KABUKA** your presence is therefore required on the date and the time indicated.
**Given under my hand and the seal of the court this 10 th day of DECEMBER,2021**

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

**RESIDENT MAGISTRATE**
**BUKOBA**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**LAND CASE APPLICATION NO 34 OF 2021**
**(Original from DLTH Karagwe Misc,Application No 65 of 2020 & Civil Case No.07 of 2016 0f Nyaishozi Ward Tribunal)**

**EMMANUEL M. BASHUNGA.....................APPELLANT**
**VERSUS**
**JOSEPH BAGARAGAZA .......................RESPONDENT**

**TO:JOSEPH BAGARAGAZA**
**KARAGWE**

**REF:NOTICE OF DATE OF HEARING**

Whereas the above mentioned appellant lodged Appeal against your and registered as Land Case Application No 34 of 2021.
Take notice that the above said case has been fixed for hearing on 5/01/2022 at 9.00 am before Hon Emmanuel L. Ngigwana,Judge your authorized to appeal in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date time for the said hearing the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 8th day of Dec,2021

**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT OF TANZANIA**
**BUKOBA**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

RASHID ABDUL KASHOBA anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki namba MC488 AXK.Taarifa imetolewa katika kituo cha Polisi Bukoba na yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.Taarifa ya Polisi ni Kumb KAG/BUK/555720/2021

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

KAYOMBO HOSEA MAJOGORO
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T320BTH ,
Engine No ISZ0952382
Chassis No. CSP110057747
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/601194/2021.

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-6

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Akamsogelea alipokuwa akijifuta vumbi. "Unaweza kurekebisha hali hii." Aliambiwa, lakini hakuelewa.

"Huyu aliyekupiga, ukitaka unaweza kumpiga." Aliambiwa tena na yule kijana, kwa mbali ni kama alianza kumuelewa.

"Naweza kumpiga kivipi?" Aliuliza.

"Mimi nafanya mazoezi kwa master wetu Zedi, anatufundisha sanaa za mapigani, staili mbalimbali, kama unataka twende ukajiunge ujifunze. Siyo kwa ajili ya kuonea watu, ila kwa ajili ya kujilinda."

Ni siku hiyo hiyo ambayo Jan alijiunga na kambi hiyo iliyopo Kinondoni Moscow, baada ya miezi minne tu, alikuwa mahiri kwenye karate, kungfu na hata kutumia silaha za jadi kama mkuki, mshale, cheni, vijiti na fimbo.

Ziliwashangaza wengi, wote waliokuwa wanampiga, aliwakung'uta kwa pigo moja tu. Alichogundua kuwa kumbe waliokuwa wanamuonea ni watu ambao hawakuwa fiti kabisa, ni kwamba jinsi alivyo hatakiwi kupigana nao, badala yake anatakiwa kupigana na watu ambao wana ujuzi na mapigano.

Hadi leo hajaacha mazoezi ya sanaa za mapigano. Ni mchezo aliotokea kuupenda sana.

Alikuwa juu ya pikipiki yake aina ya Yamaha, bomba mbili ambayo aliletewa zawadi na mzungu mmoja rafiki yake, baada ya kumtengenezea pikipiki zake, alielekea Ubungo kwa Diana. Ni yule msichana aliyemsaidia kumrudishia mkoba wake ulioporwa na kibaka.

"Ananiitia nini huyu demu?" Alijiuliza.

"Ndiyo, usiwe na wasiwasi Jan, mimi naishi kwa mjomba wangu, sijaolewa wala sina mambo mengi, nakwita kama rafiki yangu ambaye siku ile umenisaidia sana, nataka nitoe shukurani kwako, niwaonyeshe na ndugu zangu kijana aliyenisaidia, tule chakula cha mchana wote, basi, na mimi nikuonyeshe uungwana." Akakumbuka alivyojibiwa.

"Ahaa, ni kulipa fadhila." Alijikumbusha.

"Sijaolewa na wala sina mambo mengi." Ni moja kati ya jibu alilopewa ambalo alijiuliza maana yake.

"Inawezekana alidhani naweza kuogopa kwenda kwa sababu labda ana mume au mpenzi."




**Awali alikataa, lakini vizawadi vya hapa na pale na kuhakikishiwa maisha bora. Bishada aliona akikubali kutembea na mzee Khan basi maisha ya manyanyaso yatakuwa yameisha mle ndani. Akakubali.**

Jan hakutaka kujidanganya moyoni mwake kutaka kumpenda Diana. Ni msichana mzuri, mrembo wa warembo, lakini alijua hana uwezo wa kummiliki.

Ni msichana na hadhi ya juu ambaye wenye uwezo mkubwa ndiyo wanaoweza kupishana kumgombea na si yeye.

Hata hivyo alikiri kuwa ni msichana ambaye mwanaume yoyote yule angependa kuwa ubavuni kwake.

Kitendo tu cha kuitwa na msichana yule, nyumbani kwao, pekee kilitosha kumfanya ajisikie vizuri. Ajisikie faraja na kuthaminiwa, kwani si kawaida na ni mara chache kwa wasichana wenye urembo wa aina ile kuwa na tabia hiyo, hasa kwa mwanaume wa kawaida kama yeye 'fundi mapikipiki'.

*************************

"Mjomba huyu ndiye yule kijana ambaye alinisaidia baada ya kukabwa na vibaka." Diana alimweleza mjomba wake.

"Karibu kijana, sijike uko nyumbani." Mjomba alimkaribisha.

Diana alikuwa amemdanganya mjomba wake. Badala ya kumwambia alimkimbiza mwizi na kuuchukua mkoba ambaye alikuwa ameporwa, yeye alimwambia kuwa alivamiwa na vibaka wanne, kijana huyo akajitokeza na kuwapiga wote na kukimbia.

Ilikuwa ni nia ya Diana kumfanya mjomba wake kukubali ujio wa Jan, vinginevyo aliona asingekubali.

Wakati chakula kikitengenezwa. Ni Diana aliyebaki na Jan na kuzungumza mengi.

Jan alimuelezea historia nzima ya maisha yake.

"Pole sana, ilitaka kufanana na ya kwangu tu, ila mimi nitakusimulia historia ya maisha yangu, tangu mama yangu.

*******************

Kwa umri wa miaka 25 aliyonayo sasa ameshaona mengi. Ameshakutana na wanaume wa aina tofauti. Wenye mbinu tofauti za kutongoza wanawake.

Kifupi ni kwamba Diana alijua thamani ya uzuri wake tangu akiwa kinda. Alipotimiza miaka 15 tu, tayari wanaume wenye tamaa walianza kummezea mate.

Labda uzuri wake ulitokana na mchanganyiko wa damu ya kibantu na kihindi. Mama yake alikuwa mfanyakazi wa ndani kwa mzee mmoja wa kihindi mjini Mbeya.

Wakati mama wa kihindi hayupo, mzee Khan alikuwa akichombeza hapa na pale kwa mama yake Diana.

Awali alikataa, lakini vizawadi vya hapa na pale na kuhakikishiwa maisha bora. Bishada aliona akikubali kutembea na mzee Khan basi maisha ya manyanyaso yatakuwa yameisha mle ndani. Akakubali.

Na kweli ikawa hivyo. Mshahara wake ukaongezwa na akawa hacheleweshwi. Biashada akawa kama malkia mdogo kwenye nyumba ya mzee Khan, licha ya kwamba alikuwa akiingia asubuhi na kuondoka nyumbani jioni.

Wale wahenga waliosema penzi halina siri wala hawakukosea. Kuna waliosema penzi halisikiki, ila linaonekana. Mama wa kihindi akaanza kuhisi kuwa kuna mchezo ambao hauelewi unachezwa baina ya mumewe na binti wa kazi.

Alichofanya, akachachamaa hadi binti akatimuliwa kazi. Kwa bahati mbaya tayari alikuwa mjamzito. Mzee Khan alikuwa ameshaonja asali, akataka kuchonga mzinga. Alimpangia chumba sehemu. Akawa anakwenda kwa kujiiba kwa Bishada. Mtoto wa watu kitumbo nde.

Ujauzito haukuwa tatizo sana kwa mzee Khan na Bishada. Waliambiana tu iwe siri, Bishada asimtaje baba wa mtoto, ila atamhudumia hadi ajifungue na mtoto atatunzwa kama kawaida. Ng'ombe wa masikini hazai. Mwezi mmoja tu kabla ya kujifungua, mzee Khan alipata ajali mbaya ya gari, ikawa mwisho wa Bishada kutesa. Tukio hilo liliumuumiza mno Bishada. Ikawa ndiyo mwanzo wa mateso. Alijifungua mtoto kwa tabu. Matunzo yake pia alikuwa ya mashaka mashaka. Hata hivyo kila mmoja alijua kuwa mtoto wa kike ambaye Bishada alijifungua atakuwa msichana mrembo kutokana na rangi ya ngozi yake na sura yake pia. Na kila alipozidi kukua, ndipo uzuri ulipojitokeza dhahiri. Mtoto huyo alipewa jina la Diana. Hadi leo hii hakuna ndugu yoyote wa Bishada aliyejua baba wa mtoto huyo, ingawa tu waliambiwa ni mzee mmoja mwenye asili ya kihindi na ameshafariki dunia.

Umbile la Diana alilichukua kwa mama yake. Ni la kibantu, alikuwa na shepu halisi ya kiafrika. Umbo namba nane. Sura yake kwa mbali ilienda upande wa pili. Ilikuwa ni ya kiasia. Nywele nyingi hadi mgongoni, zilionekana kuwa amechukua kutoka upande wa baba. Ngozi nyeupe, pua iliyochongoka, vilimfanya Diana awe tofauti na warembo wengine.

Anapopita popote pale kila mmoja ni lazima amtazame mara mbilimbili. Labda kwa mtu ambaye hajamuona. Uzuri wale haukuwashangaza wanaume tu. Hata wanawake wenzake. Walishangaa kuona msichana wa kibantu mwenye nywele ndefu kiasi kile, weupe, sura na pua kama ya kihindi.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# CHILUNDA, ZAYD KAMILI KUIVAA SIMBA SC BARA

**Na Saada Akida**

HUKU ukitangaza utaweka wazi usajili wake mpya ifikapo Januari, mwakani, uongozi wa Azam FC, umesema tayari wamekamilisha mchakato wa kuwarejesha kikosini nyota wake wawili, Yahya Zayd na Shaban Chilunda, kwa ajili ya kuiboresha timu hiyo.

**Nyota hao kwa sasa wako huru baada ya mikataba yao kufikia tamati, Chilunda aliyekuwa Morocco akiichezea Without Club na Zayd alikuwa Pharco FC ya nchini Misri.**

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema wachezaji hao wameshasaini mikataba mipya ya kuitumikia Azam FC na wanaamini wataisaidia vyema timu hiyo kama walivyokuwa kabla ya kuondoka nchini.

"Chilunda, Zayd na wale wachezaji kutoka timu ya vijana ambao walitolewa kwa mkopo akiwamo, Paulo Peter ni miongoni mwa wachezaji wanaotarajiwa kurejeshwa katika kikosi cha Azam FC," kilisema chanzo chetu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddy Abubakar, alisema kwa sasa wanapambana kutafuta matokeo mazuri huku wakiendelea kukiimarisha kikosi chao kuelekea mechi ijayo ambayo watacheza dhidi ya Simba. Iddy alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kutokana na historia ya timu hizo kila zinapokutana kuonyesha ushindani wa kusaka matokeo chanya.

Alisema kila timu hushuka uwanjani kwa lengo la kupata ushindi, hivyo wachezaji hujituma na kuonyesha kiwango bora ili kufikia malengo.

"Kulingana na mechi hizi mbili chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Abdihamid Moallin, tunatarajia kwa kiwango kilichoonyeshwa dhidi ya Ruvu Shooting tuna matarajio makubwa ya kufanya vizuri kwenye mchezo ujao dhidi ya Simba,".

"Tutakapomaliza mchezo huo, kocha (Moallin), atapitia ripoti iliyoachwa na George Lwandamina, ili kuangalia mapungufu ya timu yetu ikiwa chini yake na kufanyia kazi katika usajili huu," alisema kocha huyo.

Azam FC itawafuata Simba katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa Januari Mosi, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.




Mshindi wa SportPesa Jackpot bonus, Baraka Shoki kutoka Kanyigo, Kagera akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 18.8 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni Sh. milioni 804.6. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Taifa Jang'ombe yaitisha Yanga*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Taifa Jang'ombe imesema inatumia vyema michezo ya Ligi Kuu Zanzibar kujiandaa na mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambapo mechi yake ya kwanza watavaana na Yanga kutoka jijini Dar es Salaam.

Mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanatarajiwa kufanyika kuanzia Januari 3, mwakani na yatashirikisha timu 10 kutoka Tanzania Bara na Visiwani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Taifa Jang'ombe, Omar Khamis "Matu" alisema anaamini mechi za ligi zitaendelea kuwaimarisha wachezaji wake ili kukabiliana na ushindani katika mchezo wao dhidi ya Yanga.

Matu alisema Taifa Jang'ombe imejipanga kufanya vyema kwenye michuano hiyo na sio kushiriki kama ilivyozoeleka kwa timu zinazotoka Zanzibar.

"Tumejipanga kufanya vizuri katika michuano hii ambayo inashirikisha timu kubwa kutoka Tanzania Bara, tumejipanga kushiriki kikweli kweli na kuchukua ubingwa ikiwezekana," alisema Matu.

Aliongeza katika michuano hatatumia wachezaji wapya ambao watasajiliwa katika dirisha dogo kwa sababu anahitaji kuendelea kuwaimarisha nyota wake waliozoeana.

Taifa Jang'ombe imepangwa Kundi B pamoja na Yanga na KMKM huku Kundi A likiwa na Azam, Namungo, Yosso Boys na Meli 4 City wakati Kundi C linaundwa na Simba, Mlandege na Selem View.

## Odhiambo aitega Biashara United

**Na Saada Akida**

HUKU kukiwa na tetesi anakaribia kujiunga na Geita Gold FC, Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo, amesema yeye bado ni mwalimu wa timu hiyo ila kwa sasa yuko kwao Kenya kwa ruhusa maalumu.

Odhiambo aliliambia gazeti hili bado ana mkataba na Biashara United na amekwenda kwao kwa kufanya makubaliano na mabosi wake. Taarifa zinasema kwa sasa kikosi cha Biashara United ambacho kesho kitaikabili Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, kiko chini ya makocha wasaidizi pamoja na Mkurugenzi wa Ufundi wa timu hiyo.

Gazeti hili lilimtafuta Odhiambo ambaye alikiri yuko kwao Kenya na sababu iliyomfanya aondoke ni kutofanyiwa kazi majadiliano aliyofanya na mabosi wa timu hiyo.

"Sijamaliza mkataba, nimekuja nyumbani baada ya kutofikia makubaliano katika masuala fulani ambayo ni siri kwangu na viongozi, siwezi kusema nimeondoka au nimeacha kuinoa Biashara United, mambo yakiwa sawa wiki ijayo nitarejea Tanzania," alisema Odhiambo.

Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, hakutaka kuweka wazi juu ya uamuzi wa kocha huyo kurejea kwao.

## Simba Queens kuendeleza dozi

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuanza msimu wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kibabe, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema anaendelea kuiandaa timu yake kutafuta ushindi katika kila mechi iliyopo mbele yao.

Simba Queens ambao ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo walianza msimu mpya kwa kutoa kichapo cha bila huruma cha mabao 15-0 kwa Ruvuma Queens hapo juzi.

Nkoma alisema malengo yake kwa sasa ni kutetea taji hilo ingawa anafahamu haitakuwa kazi rahisi kutokana na kila timu kujipanga vyema.

"Hatutaangalia timu au majina ya wachezaji wa wapinzani wetu, tunapopata nafasi tutahakikisha tunaitumia ipasavyo ili kupata mabao mengi na pointi tatu muhimu," alisema Nkoma.

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha mchezo mzuri na amewataka wasibweteke kuelekea mechi inayofuata ambayo itachezwa Jumanne dhidi ya Oysterbay Girls.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BARCA, SEVILA VITANI

KLABU ya Sevilla imejiunga na Barcelona katika kinyang'anyiro cha usajili wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani, 34. ***(Mundo Deportivo)***

### ZIYECHI ATAKIWA MILAN

AC Milan wana matumaini ya kumsajili winga wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Morocco, Hakim Ziyech, 28. ***(Calciomercato)***

### CAMAVINGA KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanapania kumnunua kiungo wa kati wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Eduardo Camavinga, 19. ***(El Nacional)***

### DEMBELE ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imewasiliana na wawakilishi wa mshambuliaji wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele, 24, ingawa klabu hiyo ya Hispania inajaribu kurefusha mkataba wake. ***(Fabrizio Romano)***

### SPURS YAMWINDA LIGT

TOTTENHAM Hotspur wanatathimini uwezekano wa kumnunua beki wa Juventus na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt, 22. ***(4-4-2 via Sun)***

### NKETIAH NJIA MOJA

KIUNGO wa kimataifa wa England na Arsenal, Eddie Nketiah, 22, anataka kuondoka kwa ajili ya kutaka kucheza katika kikosi cha kwanza licha ya washikabunduki hao kudhamiria kumwongezea mkataba. ***(Mail)***

### MARTIAL ANUKIA JUVE

KLABU ya Juventus inataka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial, 26, na mshambuliaji wa Arsenal na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (32). ***(Gazzetta dello Sport)***

### CONTE AMZUIA BERGWIJN

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte ameamua kubakia na winga wa Uholanzi, Steven Bergwijn, 24, katika klabu hiyo licha ya klabu kadhaa kumwania. ***(Sky Sports)***

### CHELSEA YAMFUATA DEST

CHELSEA wana nia ya kumsajili mlinzi wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Marekani, Sergino Dest, 21. ***(El Nacional - via Metro).***

### KESSIE AGOMBEWA ULAYA

TOTTENHAM Hotspur kwa sasa wanaongoza katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa kati wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie, 25. Timu hiyo ya Kaskazini mwa London italazimika kupambana na Paris St-Germain, ambao pia wanamtaka mchezaji huyo. ***(Calciomercato)***

### MITROVIC KUTUA MILAN

AC Milan imeonyesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Fulham ambaye pia ni raia wa Serbia, Aleksandar Mitrovic, 27. ***(90 Mins)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HATIMAYE DEMBELE KUBAKIA BARCELONA

●●● Mkataba mpya wa Mfaransa huyo utamfanya akae klabuni hapo hadi...

**BARCELONA,** Hispania

BAADA ya mvutano wa muda mrefu wa mazungumzo ya mkataba mpya kati ya Barcelona na Ousmane Dembele, taarifa zinasema hatimaye nyota huyo raia wa Ufaransa amefanya uamuzi wa kubakia klabuni hapo.

Mkataba wa sasa wa Dembele unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na klabu hiyo ilikuwa ikipambana kuhakikisha haendi kokote.

**Kwa wiki kadhaa mazungumzo kati ya pande hizo mbili yamekuwa yakiendelea, Barcelona wakiwa katika nafasi mbaya ya kutoa ofa bora zaidi kutokana na hali yao mbaya ya kiuchumi kwa sasa.**

Hata hivyo, kwa mujibu wa Footmercato, Dembele ameamua kusalia klabuni hapo kwa mkataba wa muda mrefu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo Dembele tayari ameshazungumza na wakala wake akamilishe mchakato huo ili asaini mkataba mpya wa kusalia Barcelona hadi mwaka 2024.

Uamuzi wa kuongeza mkataba kwa miaka miwili utawapa Barcelona fursa ya kutompoteza nyota huyo waliyewekeza euro milioni 130, ambaye anatajwa kuwa sehemu muhimu ya mipango ya Kocha Xavi Hernandez.


CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 804

MECHI KALI
HOME
AWAY
ENPPI CLUB
4.63 | 3.40 | 1.77
PYRAMIDS

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AUBAMEYANG KUTOLEWA KWA MKOPO



**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang anafikiria iwapo aondoke klabuni hapo ifikapo Januari baada ya kuvuliwa unahodha wiki iliyopita.

Tovuti ya soka ya Football London imesema washika bunduki hao wanapokea ofa kwa ajili ya nahodha wao huyo wa zamani, ambaye hana uhusiano mzuri na kocha, Mikel Arteta.

Arsenal inapanga kumuuza nyota huyo wa kimataifa wa Gabon ili kuepuka kutokea tena kwa balaa kama ilivyokuwa kwa Mesut Ozil msimu uliopita.

Aubameyang anatakiwa na miamba kadhaa barani Ulaya ambayo inaweza kuvutiwa kumsajili kwa mkopo.

Barcelona, Paris Saint-Germain, Juventus na AC Milan zote zinapiga rada kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kuelekea dirisha la usajili la majira ya baridi.

# Ziyech atemwa Morocco ya AFCON

**LONDON,** England

NYOTA wa Chelsea, Hakim Ziyech hatasafiri kwenda Afrika kuliwakilisha taifa lake la Morocco kwa sababu kocha mkuu wa timu hiyo, Vahid Halilhodzic hajamjumuisha kwenye kikosi chake kitakachoshiriki michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022).

Hakim hajaiwakilisha Morocco tangu Juni, mwaka huu na alijikuta akiingia kwenye mgogoro na Halilhodzic akimshutumu kwa kudanganya kuwa ameumia ili kukwepa kucheza mchezo wa kirafiki.


Ugomvi kati ya Hakim na Halilhodzic ulianza pale alipokataa kupasha misuli moto kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Ghana ambapo alidai bado anajeraha ingawa daktari wa timu ya taifa alithibisha kuwa yuko fiti. Ziyech alipewa nafasi katika mchezo uliofuata dhidi ya Burkina Faso, lakini baada ya hapo hajafanikiwa tena kuiwakilisha Morocco huku Halilhodzic akiendelea kumtuhumu kuwa hajitoi kwa asilimia 100.

Mchezaji huyo amekosa michezo 10 hadi sasa kwenye timu hiyo ya taifa na namba inatarajiwa kuzidi baada ya kuachwa kwenye kikosi ambacho kinaenda kushiriki michuano hiyo mikubwa ya Afrika.

Michuano ya AFCON inatarajiwa kuanza mwanzoni mwa Januari mwakani na kumalizika Februari.



HABARI MICHEZO



# MINZIRO : GEITA GOLD FC TUMEWASHA MOTO BARA

**Na Dennis Fussi**

KOCHA wa Geita Gold FC, Fred Minziro, amesema kikosi chake kitaendeleza 'moto' wa kufanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, kwa sababu kimeshaanza kuimarika.

Minziro alisema anaamini kilichokua kinasumbua kwenye kikosi cha Geita Gold ni hali ya wachezaji wake kutojiamini lakini sasa wameshaizoea ligi na wameanza kupata uzoefu kwa asilimia kubwa.

Kocha huyo alisema pia usajili wa baadhi ya wachezaji katika dirisha dogo lililofunguliwa umeongeza chachu ya mapambano katika kikosi hicho.

"Timu yangu sasa itaingia kwenye kiwango cha kupata ushindi, kama ambavyo unajua nilichukua timu na tukapata michezo migumu tukiwa Dar es Salaam, tulivyorudi nyumbani mambo yakawa sawa,".

"Kuna wachezaji wapya wameingia kwenye timu, hilo nalo limeongeza kitu kwenye kikosi na naona sasa tunaenda kufanya vizuri katika michezo yote inayokuja, tukianzia hapa kwetu," alisema Minziro.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Geita Gold FC ipo nafasi ya tisa ikiwa na pointi 11 baada ya kushuka dimbani michezo 10.

Kikosi hicho sasa kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya Mbeya Kwanza itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu iliyoko mkoani Geita.



Mchezaji wa Fountain Gate FC, Sadick Ramadhani (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Pan African, Maulid Jumanne, katika mechi ya Ligi ya Championship iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Fountain Gate ilishinda mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Mkwasa ataja kilichoiangusha Ruvu*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, amesema udhaifu wa wachezaji wake katika kukaba, nyota sita kwenda katika mafunzo ya kijeshi pamoja na wengine wakiwa wagonjwa, ndio kulikosababisha wapoteze mechi yao ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Azam FC iliyochezwa juzi.

Ikiwa ugenini, Ruvu Shooting ilichapwa mabao 4-1 na wenyeji Azam FC, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

"Tuliwaachia sana nafasi, tulikuwa hatukabi, tunasubiri wapate mpira ndiyo na sisi tunaanza kuwafukuza, kitu ambacho kiliwafanya wawe huru na mpira, wakawa na uwezo wa kuamua watoe pasi au wapige mashuti na hiyo ilitugharimu," alisema Mkwasa.

Kocha huyo alisema ataendelea kuwaimarisha wachezaji waliobakia ili warejee kwenye ubora wao katika mechi zinazofuata.

"Kama unavyoona leo kuna kipa mwingine, Makaka (Mohamed) ni mgonjwa, kwa hiyo tulikuwa na matatizo mengi, ndiyo maana nilijua huenda tungepoteza mechi hii, lakini si kwa idadi kubwa hivi," Mkwasa alisema.

Kichapo hicho kinaifanya Ruvu Shooting iteremke hadi katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza mechi 10 na mkononi imebakiwa na pointi tisa wakati Azam FC yenye pointi 15 ikisogea hadi nafasi ya sita.


4,667,160 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/2021 | 18:00 | Hull City vs Blackburn | 2.99 | 3.18 | 2.32 |
| 02. 26/12/2021 | 18:00 | Lincoln vs MK Dons | 2.89 | 3.29 | 2.32 |
| 03. 26/12/2021 | 18:00 | Cheltenham vs Plymouth | 2.90 | 3.34 | 2.29 |
| 04. 26/12/2021 | 18:00 | Fleetwood Town vs Shrewsbury | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 05. 26/12/2021 | 18:00 | Motherwell vs Livingston | 2.27 | 3.11 | 3.20 |
| 06. 26/12/2021 | 18:00 | Dundee Utd vs Hibernian | 3.30 | 3.11 | 2.22 |
| 07. 26/12/2021 | 18:00 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.71 | 3.40 | 2.43 |
| 08. 26/12/2021 | 18:00 | Inverness vs Partick Thisle | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 09. 26/12/2021 | 18:00 | Hamilton vs Kilmarnock | 3.11 | 3.26 | 2.19 |
| 10. 26/12/2021 | 18:00 | Ayr United vs Raith Rovers | 3.04 | 3.14 | 2.29 |
| 11. 26/12/2021 | 18:00 | Morton vs Queen of South | 2.56 | 3.30 | 2.56 |
| 12. 26/12/2021 | 18:00 | Albion Rovers vs Stranraer | 2.60 | 3.17 | 2.50 |
| 13. 26/12/2021 | 18:00 | Alfreton vs Boston Utd | 2.46 | 3.23 | 2.60 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 25 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2706 | Esteghlal Mollasani vs Saipa Karadj | 2.36 | 2.60 | 3.42 |
| 13:30 | 2972 | Shahrdari Hamedan vs Kheybar Khorramabad FC | 2.70 | 2.60 | 2.89 |
| 13:30 | 3009 | Rayka Babol vs Shahrdari Astara | 2.13 | 2.65 | 3.95 |
| 13:30 | 4267 | Erzurum BB vs Denizlispor | 1.57 | 3.82 | 5.02 |
| 13:30 | 4430 | Kasimpasa vs Altay | 2.22 | 3.41 | 3.01 |
| 13:30 | 4563 | Arman Gohar Sirjan vs Mes Shahr-e Babak | 1.85 | 2.90 | 4.64 |
| 13:30 | 4627 | Ghasghaei Shiraz vs Sanat Mes Kerman FC | 2.21 | 2.65 | 3.71 |
| 13:30 | 5330 | Malavan Bandar Anzali vs Khosheh Talaei | 1.84 | 2.86 | 4.84 |
| 13:30 | 5525 | Shahin Bushehr vs Shams Azar Qazvin | 2.70 | 2.60 | 2.89 |
| 13:30 | 5774 | Vista Turbine vs Esteghlal Khuzestan | 2.85 | 2.80 | 2.85 |
| 15:30 | 1132 | Indonesia vs Singapore | 2.15 | 3.13 | 3.18 |
| 15:40 | 1043 | Dhamk vs AL Baten | 1.91 | 3.47 | 3.86 |
| 15:45 | 1398 | Dubba Al-Husun vs Al-Hamriyah | 2.48 | 3.95 | 2.48 |
| 16:00 | 1703 | WA Boufarik vs CRB Ain Ouessara | 2.01 | 3.00 | 3.72 |
| 16:00 | 2283 | Galatasaray vs Antalyaspor | 1.57 | 3.96 | 5.35 |
| 16:00 | 2679 | Islami Qalqilya vs Hilal Al-Quds | 2.40 | 3.20 | 3.00 |
| 16:00 | 2969 | GC Mascara vs ZR Temouchent | 1.78 | 3.13 | 4.53 |
| 16:00 | 3162 | USM Bel Abbes vs Ben Aknoun | 2.37 | 2.90 | 3.00 |
| 16:00 | 3257 | CA Batna vs Hamra Annaba | 1.78 | 3.23 | 4.34 |
| 16:00 | 3428 | USM Annaba vs JSM Bejaia | 2.70 | 3.23 | 2.38 |
| 16:00 | 3511 | ASM Oran vs MC Saida | 1.93 | 3.13 | 3.80 |
| 16:00 | 3844 | Hapoel Haifa vs FC Ashdod | 2.18 | 3.14 | 3.09 |
| 16:00 | 4219 | Ajman Club vs Al Wasl Dubai | 2.85 | 3.57 | 2.13 |
| 16:00 | 4468 | Mosaset AL Bireh vs Shabab Alsamu | 2.80 | 3.10 | 2.65 |
| 16:00 | 4586 | MO Bejaia vs MC EL Eulma | 1.50 | 3.85 | 5.77 |
| 16:00 | 4739 | Giresunspor vs Hatayspor | 2.10 | 3.30 | 3.39 |
| 16:00 | 4749 | MO Constantine vs Irb Ouargla | 2.45 | 2.89 | 2.89 |
| 16:00 | 4795 | Jazira Abu Dhabi vs AL Khaleej Khor Fakkan | 1.38 | 4.72 | 6.16 |
| 16:00 | 5150 | El Bayadh vs RC Kouba | 1.78 | 3.13 | 4.53 |
| 16:00 | 5216 | US Chaouia vs Ain M'lila | 1.78 | 3.23 | 4.34 |
| 16:00 | 5843 | Enppi Club vs Pyramids | 4.63 | 3.40 | 1.77 |
| 16:05 | 3563 | Umm-Salal SC vs Lekhwiya SC | 8.05 | 5.56 | 1.26 |
| 16:05 | 3950 | Al Sadd SC vs Al Khoor | 1.02 | 11.58 | 27.98 |
| 17:50 | 5781 | Al Hilal Riyadh vs Al Fateh (KSA) | 1.59 | 4.07 | 5.16 |
| 17:55 | 2075 | AL Faiha vs Abha | 2.01 | 3.31 | 3.71 |
| 18:00 | 1122 | Smouha Club vs Talaea El Gaish | 1.90 | 3.25 | 4.14 |
| 18:00 | 2195 | Hassania Agadir vs Jeunesse Sportive Soualem | 2.13 | 3.03 | 3.32 |
| 18:15 | 1419 | Al Gharafa SC vs Al Arabi Doha SC | 2.36 | 3.43 | 2.61 |
| 18:30 | 1918 | AL Urooba vs Emirates Club | 1.95 | 3.43 | 3.38 |
| 18:30 | 4062 | Hapoel Tel Aviv vs Ironi Kiryat Shmona | 2.02 | 3.13 | 3.51 |
| 18:30 | 5355 | Al Ain vs Al Nasr Dubai | 2.01 | 3.42 | 3.23 |
| 18:45 | 1430 | Al Fehaheel vs AL Tadamon | 2.22 | 3.37 | 2.84 |
| 19:00 | 2667 | Markez Tulkarm vs Markez Balata | 4.40 | 3.90 | 1.74 |
| 19:00 | 2670 | Nazareth Ilit vs Maccabi Netanya | 2.94 | 3.04 | 2.32 |
| 19:00 | 4189 | Trabzonspor vs Basaksehir | 2.10 | 3.44 | 3.24 |
| 19:00 | 4555 | Menemen Bld vs Bursaspor | 2.84 | 3.32 | 2.24 |
| 20:15 | 2881 | Rapide Oued Zem vs FUS Rabat | 2.70 | 2.84 | 2.65 |
| 20:50 | 3796 | Bnei Sakhnin vs Maccabi Haifa | 4.81 | 3.80 | 1.59 |
| 21:00 | 4550 | Zamalek vs Ghazl EL Mahallah | 1.26 | 5.34 | 10.88 |
| 22:30 | 3019 | MAS Maghrib A Fes vs Ittihad Tanger | 2.27 | 2.94 | 3.13 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Desemba 25, 2021

Nipashe




Aubameyang kutolewa kwa mkopo UKURASA 22



Beki wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' (kulia), akifunga bao huku golikipa wa KMC, Farouk Shikalo, akiruka bila mafanikio kudaka mpira katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora jana. Simba ilishinda mabao 4-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba X-mass tamu

## ●●● Ni baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 4-1 huku Kibu...

**Na Adam Fungamwangwo**

MABAO mawili yaliyofungwa na straika aliyesajiliwa msimu huu kutoka Mbeya City, Kibu Dennis na mengine yaliyofungwa na mabeki, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' na Joash Onyango, yametosha kuifanya Simba kuibuka na ushindi wa magoli 4-1 dhidi ya KMC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora jana.

**Kibu amefikisha mabao matatu katika orodha ya wafungaji Ligi Kuu, huku Zimbwe na Onyango kila mmoja akifunga bao la kwanza msimu huu.**

Ulikuwa ni ushindi wa kwanza mnono zaidi wa Simba tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Ushindi mkubwa zaidi wa Simba kuupata msimu huu kabla wa jana ulikuwa ni Novemba 10, mwaka huu walipoifunga Ruvu Shooting mabao 3-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Matokeo hayo yanaifanya kuendelea kujikita kwenye nafasi ya pili, ikifikisha pointi 21, pointi mbili nyuma ya vinara Yanga yenye pointi 23, timu zote zimecheza mechi tisa.

Dakika ya sita tu ya mchezo, Simba ilibisha hodi langoni mwa KMC, baada ya Pape Sakho kuambaa na mpira katika winga ya kushoto na kupiga krosi iliyowahiwa na Kipa, Farouk Shikalo.

Dakika ya 10, Zimbwe Jr aliiandikia Simba bao la kwanza baada ya kukimbilia faulo iliyopigwa na Jonas Mkude, iliyotokana na Sakho kuangushwa karibu na katikati ya uwanja, akiwa pembeni upande wa kushoto, mfungaji aliunyanyua mpira kama anapiga krosi, mpira ukaenda moja kwa moja wavuni na kumwacha Farouk akiruka bila mafanikio.

Zilipita dakika mbili kabla ya Onyango kupachika bao la pili kwa kichwa, alipounganisha kona iliyopigwa na Rally Bwalya.

Baada ya mabao hayo mawili ya haraka, ni kama wachezaji wa Simba waliridhika na kuwaacha KMC kutawala mechi hiyo, ikishuhudia dakika ya 21, Emmanuel Mvuyekule akikosa bao la wazi, baada ya kuupata mpira akiwa ndani ya eneo la hatari, lakini alikosa utulivu na mabeki wa Simba wakafanikiwa kuokoa.

Alikuwa ni Abrulrazack Mohammed aliyewarudisha mchezoni KMC kwa kupachika bao safi akiwa pembeni kidogo ya lango la Simba, akitumia makosa ya walinzi wa timu hiyo 'kukaba kwa macho', baada ya kupata krosi ndefu kutoka kwa Ken Mwambungu na kupiga shuti dhaifu, lakini la kiufundi lililojaa wavuni dakika ya 39.

Kipindi cha pili, Simba iliingia kama mbogo aliyejeruhiwa, na dakika mbili tu baada mechi kuanza, ilipachika goli la tatu, mfungaji akiwa ni Kibu.

Ulikuwa ni mpira wa faulo aliyechezea Shomari Kapombe na yeye mwenyewe kupiga faulo iliyodondoka kwenye 'msitu' wa wachezaji wa pande zote mbili, Kibu akapiga shuti la kushtukiza lililojaa wavuni na kumwacha kwa mara nyingine, Farouk akiruka bila mafanikio.

Kibu tena, dakika ya 57, akiwa umbali wa mita 35, baada ya gonga za hapa na pale za wachezaji wa Simba, alichia kombora kali la juu, lililokwenda kukwama wavuni na kuwa bao la nne kwa timu yake hiyo.

Simba iliwatoa Sakho, Rally Bwalya na Zimbwe Jr, ikimwingiza kwa mara ya kwanza kuichezea timu hiyo, Abdulswamad Kassim aliyesajiliwa akitokea Kagera Sugar, Yusuph Mhilu na Hassan Dilunga.

Nusura KMC ipate bao dakika ya 77, baada ya Matheo Antony, kupokea krosi kutoka kwa Idd Kipwagile, akiwa hajakabwa na mabeki wa Simba, aligeuka na kuachia shuti kwa mguu wa kushoto, Aishi Manula akiwa amesimama tu, mpira ulitoka sentimeta chache langoni mwa Simba.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa jana, wenyeji Coastal Union wakiwa nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga walipata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Mbeya Kwanza.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa vinara Yanga kuwakaribisha Biashara United kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

# Yanga sasa yaibadilishia gia Biashara

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anahitaji kuchanganya vyema 'karata zake' ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga yenye pointi 23 ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara, wakati mabingwa watetezi, Simba wenyewe wanashika nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema hakuna mchezo ambao kwao wataona wa kawaida na kila siku wanaendelea kujipanga vizuri kwa kusahihisha makosa waliyoyabaini katika mechi iliyopita.

Nabi alisema hakuna mechi rahisi msimu huu na anawahimiza wachezaji wake kutobweteka kwa kuona kila mechi wanayocheza ni sawa na fainali, hivyo wanahitaji matokeo ya ushindi tu ili kujiimarisha kileleni.

"Ligi ni ngumu sana na ushindani ni mkubwa, kila timu tutakayocheza nayo inahitaji kupata matokeo chanya, sisi pia tunahitaji ushindi na tunataka kutwaa ubingwa, hakuna kudharau timu wala majina ya wachezaji wa wapinzani wetu,"

"Biashara United ni timu nzuri, ukizingatia imewahi kucheza michuano ya kimataifa, tunawaheshimu kwa sababu wana uzoefu, tumeimarisha kikosi kiufundi na kimbinu ili kwenda kupata pointi muhimu katika mchezo huo," alisema Nabi.

Aliongeza kikosi chake kitakuwa na mabadiliko makubwa huku wakicheza kwa juhudi zaidi pale wanapokuwa nyuma kwa ajili ya kusawazisha na hatimaye kupata bao la ushindi.

"Nalazimika kufanya mabadiliko kutokana na wachezaji niliobakia nao, baadhi bado wagonjwa huku wengine wakiwa ni majeruhi wanaohitaji matibabu makubwa, lakini sina wasiwasi, tutaingia kupambana ili kusaka pointi tatu na si vinginevyo," Nabi aliongeza.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >